# RIPOTI YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

FEBUARI 2023

# YALIYOMO

*SEHEMU YA KWANZA* ..... *1*

UTANGULIZI ..... 1

Muundo wa Kamati ya Bajeti ..... 2

*SEHEMU YA PILI* ..... *4*

TATHMINI YA MWENENDO WA UKUAJI WA HALI YA UCHUMI ..... 4

Mfumko wa Bei ..... 4

Mwenendo wa Sarafu ya Tanzania ..... 5

Idadi ya Watalii ..... 6

Maoni na Ushauri wa Kamati ..... 7

*SEHEMU YA TATU* ..... *8*

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/2022 NA NUSU MWAKA WA FEDHA 2022/2023 (JULAI – DISEMBA 2022/2023) ..... 8

Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2021/2022 ..... 8

Mwenendo wa Mapato na Matumizi kwa Nusu Mwaka wa 2022/2023 (Julai – Disemba 2022/2023) ..... 8

Deni la Taifa ..... 9

Maoni na Ushauri wa Kamati ..... 9

*SEHEMU YA NNE* ..... *11*

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA ..... 11

MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA) ..... 11

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA) – MKOA WA KIKODI PEMBA ..... 13

MAMLAKA YA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPRA) 16

KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA ZANZIBAR (ZPDC) ..... 17

MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA (ZPPDA) ..... 18

TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR (ZAHRI) ..... 19

WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA ZANZIBAR (ZICTIA) ..... 20

KAMPUNI YA MWANI ZANZIBAR (ZASCO) ..... 21

MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR ..... 23

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR (OCGS) ..... 24

SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR ..... 26

KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR (ZAFICO) ..... 27

SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR (ZPC) ..... 29

SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI ZANZIBAR ..... 32

MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA) ..... 33

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF) ..... 35

SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR (ZIC) 36

*SEHEMU YA TANO* *38*

**TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA PROGRAMU MBALI MBALI 38**

MIRADI NA PROGRAMU ZILIZOTEKELEZWA KWA FEDHA ZA AHUENI YA UVIKO 19 KUTOKA SHIRIKA LA FEDHA DUNIANI (IMF) 38

MRADI WA OFISI NA MAABARA YA TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS) - MARUHUBI 44

MRADI WA UJENZI WA MAREKEBISHO YA BANDARI YA MKOANI PEMBA PAMOJA MRADI WA UJENZI WA BANDARI YA SHUMBA 47

MRADI WA UIMARISHAJI ELIMU YA LAZIMA 49

MRADI WA MPANGO WA UTAYARISHAJI WA MATUMIZI YA ARDHI ZANZIBAR 50

MRADI WA UJENZI WA NYUMBA NA MAHANGA YA KMKM KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 NA 2022/2023 KWA KAMANDI YA PEMBA 51

MRADI WA UJENZI WA NYUMBA NA MAHANGA YA KVZ KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 NA 2022/2023 53

MIRADI YA TUME YA MIPANGO ZANIBAR 54

PROGRAMU YA UMWAGILIAJI MAJI KWA MWAKA 2021/2022 NA 2022/2023 56

PROGRAMU YA UJENZI WA BARABARA ZA NDANI NA MATENGENEZO YA BARABARA MJINI 57

PROGRAMU YA KUIMARISHA MAENEO YA KIHISTORIA KWA MWAKA WA FEDHA 2022 59

PROGRAMU YA KUIMARISHA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR 61

PROGRAMU YA UJENZI WA BARABARA KUU KWA BARABARA YA CHAKE CHAKE - WETE NA CHAKE CHAKE - MKOANI 62

*SEHEMU YA SITA* *65*

**TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA 65**

HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI 65

BARAZA LA MJI WETE 67

BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE 68

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKOANI 69

MANISPAA YA MJINI 71

MANISPAA YA MAGHARIBI ‘A’ 72

MANISPAA YA MAGHARIBI ‘B’ 74

BARAZA LA MJI KATI 76

HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI 78

BARAZA LA MJI KASKAZINI ‘A’ 79

BARAZA LA MJI KASKAZINI ‘B’ 81

TATHMINI YA HALI YA UKUSANYAJI WA MAPATO YATOKANAYO NA TOZO ZA MAEGESHO YALIYOPO KATIKA WILAYA YA MJINI HUSUSAN MAENEO YA MASOKO NA MAENEO MAALUM YA MAEGESHO 83

TATHMINI YA HALI YA UKUSANYAJI WA MAPATO YATOKANAYO NA BIASHARA NA HUDUMA ZITOLEWAZO KATIKA ENEO LA FORODHANI KWA MWAKA 2021/2022 85

*SEHEMU YA SABA* ........ *87*
HITIMISHO ........ 87

# SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Kamati ya Bajeti ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zilizoundwa chini ya Kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Baraza, Toleo la Mwaka 2020. Kamati hutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizo. Aidha, Kamati huzingatia Katiba, Sheria na miongozo mbali mbali ya nchi katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Majukumu ya Kamati ya Bajeti yaliyoainishwa katika Kanuni hizo ni kama ifuatavyo:

i. Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu uandaaji wa mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kila mwaka;
ii. Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;
iii. Kufanya utafiti na uchambuzi kuhusu sera za kodi, sera za fedha na sera za kiuhasibu zilizopendekezwa na Serikali;
iv. Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali na mapendekezo ya hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti;
v. Kutoa ushauri wa jumla kuhusu bajeti ya Serikali kwa Baraza na Kamati za Kudumu za Baraza;
vi. Kuchambua na kutoa maoni na ushauri kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaopendekezwa na Serikali;
vii. Kuchambua hoja zitakazojitokeza kwenye Kamati za Kudumu za Baraza wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa ajili ya kuishauri Serikali;
viii. Kuchambua mapendekezo ya jumla ya Serikali kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi;
ix. Kufikiria na kuchunguza Mswada wa Makadirio na Mapato ya matumizi ya mwaka;
x. Kuchambua mapendekezo ya Serikali endapo itataka kuwasilisha katika Baraza Mswada wa Matumizi ya Nyongeza kwa mujibu wa kanuni ya 102 ya Kanuni hizi; na
xi. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya

Kamati ya mwaka uliotangulia na kutathmini taarifa ya Wizara juu ya utekelezaji wa maagizo hayo na kuwasilisha Barazani maoni ya Kamati kuhusu taarifa hiyo.

Katika kutekeleza majukumu hayo, Kamati ilikutana na Wizara mbali mbali, Taasisi, Mamlaka, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na wadau mbalimbali kwa ajili ya kupokea taarifa za utendaji kazi na kupokea maoni mbali mbali. Katika utekelezaji wa majukumu hayo, Kamati imetoa maoni na ushauri kwa Serikali na taasisi hizo kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi pamoja na utekelezaji bora wa bajeti ya Serikali.

**Muundo wa Kamati ya Bajeti**

Kamati ya Bajeti imeundwa na Wajumbe sita (6) na Makatibu Kamati wanne (4) kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Abdulla Hussein Kombo | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi Gavu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Miraji Khamis Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 8. | Ndg. Abass Vuai Mohammed | Katibu |
| 9. | Ndg. Husna Rajab Othman | Katibu |
| 10. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |

Taarifa ya Kamati ya Bajeti imegawanyika katika Sehemu Kuu Saba (7). **Sehemu ya Kwanza** ni Utangulizi; **Sehemu ya Pili** ni Tathmini ya Mwenendo wa Ukuaji wa Hali ya Uchumi Zanzibar; **Sehemu ya Tatu** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022 na Nusu Mwaka wa fedha 2022/2023 (Julai – Disemba 2022/2023); **Sehemu ya Nne** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Taasisi na Mashirika ya Umma; **Sehemu ya Tano** ni Tathmini ya

Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; **Sehemu ya Sita** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; na **Sehemu ya Saba** ni Hitimisho.

# SEHEMU YA PILI

## TATHMINI YA MWENENDO WA UKUAJI WA HALI YA UCHUMI

### Mfumko wa Bei

Mfumko wa Bei Zanzibar umeongezeka katika mwaka 2022 na kufikia wastani wa asilimia 5.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2021. Kuongezeka kwa mfumko wa bei kumesababishwa kwa kiasi kikubwa na

kupanda kwa bei za bidhaa za chakula hususani mchele, unga wa ngano na sembe, ambapo mfumko wa bei wa bidhaa hizo za chakula umefikia wastani wa asilimia 12.6 kwa mwaka 2022. Jadweli Nam. 1 linafafanua.

**Jadweli Nam. 1: Mfumko wa Bei kwa kila mwezi kwa mwaka 2021 na 2022**

| Mwezi | Mfumko wa Bei (Asilimia) | |
|---|---|---|
| | 2021 | 2022 |
| Januari | 0.5 | 2.8 |
| Februari | 0.7 | 2.9 |
| Machi | 1.5 | 3.5 |
| Aprili | 1.9 | 4.1 |
| Mei | 0.8 | 3.7 |
| Juni | 1.9 | 4.2 |
| Julai | 2.2 | 4.5 |
| Agosti | 2.1 | 5.4 |
| Septemba | 2.4 | 7.0 |
| Oktoba | 2.1 | 7.3 |
| Novemba | 2.2 | 7.8 |
| Disemba | 2.4 | 8.1 |
| **Wastani kwa Mwaka** | **1.7** | **5.1** |

**Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (2023)**

Kuongezeka kwa kasi ya mfumko wa bei kwa mwaka 2022 kwa kiasi kikubwa kumetokana na uchumi wa dunia kuendelea kukumbana na changamoto mbali mbali zinazotokana na kupanda kwa bei za mafuta na gesi asilia katika soko la dunia. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa ruzuku katika bei ya nishati ya mafuta, jambo ambalo limesaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti mfumko wa bei katika nishati ya mafuta. Aidha, kupanda kwa gharama za usafirishaji wa mizigo inayoletwa kutoka nje ya nchi kutokana na uwezo mdogo wa bandari ya Malindi Zanzibar kuhudimia meli za mizigo. Vile vile, sekta ya usafirishaji ya dunia imeathiriwa kwa kiasi kikubwa na vita vya Ukrein na Urusi ambavyo vimekuja

baada ya dunia kukabiliana na athari za UVIKO 19 jambo ambalo limesababisha bidhaa nyingi kupanda bei hususan chakula na nishati kama vile mafuta na gesi.

### Mwenendo wa Sarafu ya Tanzania

Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani imeendelea kuwa tulivu, ambapo dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 2,308.89 katika soko la jumla katika kipindi cha Disemba mwaka 2022, ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,297.81 katika kipindi kama hicho mwaka 2021.

Aidha, Shilingi ya Tanzania ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 18.63 kwa Shilingi moja ya Kenya katika kipindi cha Disemba mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa TZS 20.22 kwa Shilingi moja ya Kenya katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Kadhalika, katika kipindi hicho cha Disemba 2022, Shilingi ya Tanzania ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 0.59 kwa shilingi moja ya Uganda ikilinganishwa na wastani wa TZS 0.62 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. **(Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania)**

### Idadi ya Watalii

Idadi ya watalii walioingia Zanzibar imeendelea kukua na kufikia 544,233 mwaka 2022 kutoka watalii 394,185 waliongia katika mwaka 2021. Jadweli Nam. 2 linafafanua.

**Jadweli Nam. 2: Idadi ya Watalii kwa kila mwezi kwa mwaka 2021 na 2022**

| Mwezi | Idadi ya Watalii | |
|---|---|---|
| | 2021 | 2022 |
| Januari | 49,868 | 42,443 |
| Februari | 51,574 | 46,995 |
| Machi | 43,821 | 38,762 |
| Aprili | 13,839 | 20,540 |
| Mei | 9,280 | 20,450 |

| | | |
|---|---|---|
| Juni | 20,416 | 34,013 |
| Julai | 29,714 | 58,157 |
| Agosti | 34,425 | 61,388 |
| Septemba | 25,817 | 46,338 |
| Oktoba | 31,826 | 57,547 |
| Novemba | 35,438 | 50,880 |
| Disemba | 48,167 | 66,720 |
| **Jumla** | **394,185** | **544,233** |

**Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (2023)**

Kuongezeka kwa idadi ya watalii katika mwaka 2022 kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na zoezi la kuitangaza Tanzania kupitia filamu ya ROYAL TOUR. Kwa dhati kabisa, Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuja na wazo hili na pia kushiriki katika kutengeneza filamu hii. Aidha, Kamati inampongeza Rais wa Zanzibar, na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, nae kwa kushiriki katika utengenezaji wa filamu hii. Aidha, sababu nyengine ambazo Kamati imebaini zimechangia kuongezeka kwa watalii ni kuwepo kwa chanjo ya UVIKO 19, ambayo imepelekea baadhi ya nchi kuondosha vikwazo vya kusafiri katika nchi zao kutokana na kupungua kwa maambukizi kwa kiwango kikubwa duniani, hali ambayo imepelekea kuanza kuimarika kwa sekta mbali mbali za kiuchumi ikiwemo sekta ya utalii ambayo inachangia asilimia kubwa katika uchumi wa nchi yetu.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa ruzuku katika nishati ya mafuta kwani inasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti mfumko wa bei wa bidhaa hiyo muhimu kwa uchumi wa nchi yetu.

ii. Kamati inaishauri Serikali kuitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto ya meli za mizigo kuchelewa kufunga gati katika Bandari ya Malindi Zanzibar ili

kupunguza gharama za usafiri kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi.

iii. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitekeleza miradi ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhia chakula, Kamati inaishauri kuendeleza miradi hiyo sambamba na kuanza kununua bidhaa za chakula na kuzihifadhi katika maghala hayo ili ziweze kusambaza chakula hicho kwa njia ya kuuza kwa bei nafuu pale ambapo bei zinapanda. Hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti mfumko wa bei kwa bidhaa za chakula.

iv. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kuifungamanisha Sekta ya Utalii na uchumi wa mwananchi mmoja mmoja. Mfano, kuwezeshwa kwa vikundi vya wajasiriamali kuzalisha bidhaa zinazotumika katika hoteli za kitalii kama vile mboga mboga, viungo vya chakula nakadhaalika. Hatua hii itasaidia kuimarisha uchumi wananchi moja kwa moja.

## SEHEMU YA TATU

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/2022 NA NUSU MWAKA WA FEDHA 2022/2023 (JULAI – DISEMBA 2022/2023)

### Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2021/2022

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 1,829.9 bilioni kati ya fedha hizo TZS 1,134.9 bilioni ni kutokana na mapato ya ndani na TZS 695.0 bilioni ni mapato mengineyo. Aidha, mapato halisi yalikuwa TZS 1,454.42 bilioni sawa na asilimia 79 ya makadirio ya mapato.

Kwa upande wa matumizi, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilikadiria kutumia jumla ya TZS 1,829.9 bilioni ikihusisha TZS 947.1 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TZS 882.8 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Aidha, matumizi halisi yalifikia TZS 1,207.1 bilioni. Kati ya matumizi hayo, TZS 740.9 bilioni zimetumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 78.2 ya makadirio ya TZS 947.1 bilioni na matumizi kwa miradi ya maendeleo yalifikia TZS 466.2 bilioni sawa na asilimia 52.8 ya makadirio ya kutumia TZS 882.8 bilioni.

## Mwenendo wa Mapato na Matumizi kwa Nusu Mwaka wa 2022/2023 (Julai – Disemba 2022/2023)

Katika kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2022/2023 (Julai – Disemba 2022/2023), Serikali imefanikiwa kukusanya TZS 659.69 bilioni sawa na asilimia 91 ya makadirio ya TZS 722.53 bilioni kwa kipindi hicho, na asilimia 26 ya makadirio ya TZS 2,572.7 bilioni kwa mwaka mzima wa 2022/2023. Matumizi halisi ni TZS 683.36 bilioni ambapo TZS 487.17 bilioni zimetumika kwa kazi za kawaida na TZS 190.69 bilioni zimetumika kwa kazi za maendeleo.

Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika kipindi cha nusu mwaka 2022/2023, mapato yamefikia jumla ya TZS 6.1 bilioni kutokana na vyanzo vyake vya ndani, makusanyo hayo sawa na asilimia 73 ya makadirio ya kukusanya TZS 8.3 bilioni kwa kipindi hicho na ni sawa na asilimia 35 ya makadirio ya mwaka nzima ya TZS 17.6 bilioni.

## Deni la Taifa

Hadi kufikia Disemba 2022, Deni la Taifa limefikia TZS 331.9 bilioni ambapo kati ya deni hilo, deni la ndani ni TZS 318.7 bilioni sawa na asilimia 96 ya deni lote na deni la nje ni TZS 13.2 bilioni sawa na asilimia 4 ya deni lote. Aidha, hadi kufikia Disemba, 2022 Deni la Nje linalodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Zanzibar limefikia TZS 2,368.1 bilioni.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kuendelea na hatua za kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na mifumo ya manunuzi kwa njia za kielektroniki ili kuendelea kudhibiti uvujaji wa mapato na kudhibiti manunuzi.
ii. Kamati inaishauri Serikali kuendelea na hatua za kudhibiti matumizi Serikalini.
iii. Serikali inaendelea kuimarika katika hatua za ukusanyaji wa mapato kwa upande wa Serikali kuu lakini bado hali ya ukusanyaji wa mapato kwa Serikali

za Mitaa haijawa ya kuridhisha. Uwezo wa watendaji katika kukusanya mapato ni mdogo na pia kumekuwepo na upotevu mkubwa wa mapato. Kamati inaishauri Serikali, kuvipitia vyanzo vyote vya kila Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuweka makadirio ya mapato kulingana na hali halisi ya kila sehemu husika.

iv. Misamaha ya kodi imekuwa ikiongezeka, mathalan katika kipindi cha Julai - Disemba 2022/2023, Misamaha ya Kodi inayotolewa na Serikali imefikia TZS 46.06 bilioni, misamaha imeongezeka kwa TZS 37.94 bilioni ikilinganishwa na misamaha ya TZS 8.12 bilioni iliyotolewa kipindi kama hicho 2021/2022. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 567.2. Kamati inaishauri Serikali, ifanye tathmini ya kina kuhusu misamaha ya kodi, kwani iwapo misamaha hiyo haichochei ukuaji wa uchumi wetu basi ni sawa na upotevu wa mapato. Je, kuna ulazima kila mwekezaji kupewa msamaha wa kodi? Msamaha utolewe pale tutakapojiridhisha kwamba utaleta tija na kuchochea uchumi wetu.

v. Kamati inaishauri Serikali kufuatilia mashirika ya umma na kampuni za Serikali kuhakikisha kwamba yanajiendesha kwa faida ili hatimae yaweze kutoa gawio kwa Serikali. Hali ilivyo kwa sasa, mashirika na kampuni hizo zimekuwa mzigo mkubwa kwa Serikali.

vi. Kamati inaishauri Serikali kutokuendelea kukopa fedha ZSSF kwa sababu majukumu ya ZSSF ni kukusanya fedha za wanachama wake na kuziweka ili iweze kupata faida.

# SEHEMU YA NNE

# TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA

Ili kubaini kiasi cha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Mashirika ya Umma, Mamlaka na Kampuni za Serikali, Kamati ya Bajeti ilizitembelea baadhi ya taasisi hizo. Tathmini ya Kamati kwa Mashirika ya Umma, Mamlaka na Kampuni za Serikali katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo ni kama ifuatavyo:

## MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA)

Mamlaka ya Mapato Zanziabr (ZRA) ina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuhakikisha kuna usimamizi mzuri wa sheria za kodi katika taasisi zote zinazohusiana na kukusanya mapato. Kamati ilitembelea Bodi ya Mapato Zanzibar ili kutathmini juu ya utekelezaji wa majukumu yake ya ukusanyaji wa Mapato.

Kwa kipindi cha Julai - Septemba 2022/2023, ZRA ilikadiriwa kukusanya TZS 135.125 bilioni kutoka vianzio vya kodi tu. Ambapo makusanyo halisi yaliyokusanywa ni TSZ 131.793 bilioni sawa na asilimia 97.53 ya makadirio. Hatua hii imejumuisha uwendelezaji wa kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa utoaji risiti za kielektroniki kwa wafanya biashara, kuanzishwa Ofisi za Mikoa pamoja na kusajiliwa walipa kodi wapya. Hii imetokana na muamko walioupata kupitia elimu zinazotolewa.

### Changamoto Zilizobainika

i. Uelewa mdogo wa wanajamii juu ya uwepo wa vituo vya huduma kwa wateja wa Mamlaka pamoja na huduma zinazotolewa na vituo hivyo.

ii. Kuwepo kwa wafanyabiashara wengi ambao hawatoi risiti za kielektroniki wanapofanya mauzo ya bidhaa na huduma zao hali inayopelekea kuikosesha Mapato Serikali.

iii. Kuwepo kwa muitikio mdogo wa wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiari unapunguza makusanyo.

iv. Kuwepo kwa tatizo la kutopatikana mtandao katika baadhi ya maeneo, hali inayopelekea kuchelewesha au kukwamisha zoezi la utoaji wa risiti kwa muda muafaka.

v. ZRA kushindwa kuunganisha mifumo ya hoteli za kitalii katika mifumo ya kodi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri ZRA kuunda kitengo maalum cha mafundi ambao watatoa msaada wa kiufundi wa haraka kwa watumiaji wa mashine za kutolea risiti ili ziweze kuchapishwa kwa wakati.

ii. Kamati inaendelea kuisisitiza ZRA kuendelea na utoaji wa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari. Suala la utoaji wa elimu liwe endelevu ili lizoeleke katika jamii hatimae yawe ni mazoea yetu kulipa kodi kwa hiari. Aidha, ZRA inatakiwa kuimarisha huduma zinazotolewa kwa walipa kodi ili kuvutia wafanyabiasha Kwenda kulipa kodi.

iii. Kamati inaishauri ZRA kufanya tafiti wa namna taasisi za kukusanya kodi katika nchi za visiwa kama Zanzibar zinavyotekeleza majukumu yao ya kukusanya kodi katika hoteli za kitalii na maeneo mengine ya kitalii ili kuongeza mbinu na ujuzi wa namna kuongeza mapato kutoka katika sekta ya utalii.

iv. Ili kuongeza makusanyo, ni vyema Serikali ikapunguza misamaha ya kodi (Tax Exemptions) isiyo na tija kwa nchi yetu. Kamati inasisitiza kuwepo kwa uwazi katika misamaha ya kodi na kutathmini upya utaratibu wake.

## MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA) – MKOA WA KIKODI PEMBA

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imekipandisha hadhi kituo cha kodi Pemba tarehe 01/07/2022 na kuwa Mkoa wa Kikodi Pemba, ufanisi katika ukusanyaji wa

mapato umevuka malengo. Hali ya makusanyo kwa nusu mwaka wa fedha 2022/2023 imefikia asilimia 104 ya malengo, ambapo lengo la makusanyo kwa kipindi hicho lilikuwa ni TZS 5.39 bilioni lakini Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) – Mkoa wa Kikodi Pemba imefanikiwa kukusanya TZS 5.62 bilioni.

Hatua hii inatia moyo sana kwa kuwa inaendana na mipango ya Serikali ya kukifanya kisiwa cha Pemba kuwa eneo maalum la kimkakati la uwekezaji, utalii na biashara. Ni matarajio ya Kamati ya Bajeti kwamba, makadirio ya mapato yataenda sambamba na upatikanaji wa fursa za kuzalisha mapato hayo, kwani fursa nyingi zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku. Aidha, ni matarajio ya Kamati kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania - Mkoa wa Kikodi Pemba kuwa makadirio ya mapato ya TZS 11.321 bilioni yaliyopangwa na Serikali katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 yatafikiwa na kuvuka kwa malengo ya makusanyo hayo.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kutokuwepo kwa mazoea ya kulipa kodi kwa hiari miongoni mwa wafanyabiashara.
ii. Ufinyu wa nafasi katika Bandari za Mkoani na Wete Pamoja na uhaba wa nyenzo za kushushia mizigo kutoka katika meli, hali ambayo inapelekea wafanyabiashara kutokuingiza mizigo moja kwa moja kutoka nje ya nchi. Hali hii inapunguza mzunguko wa biashara na kupelekea upungufu wa mapato katika kisiwa cha Pemba.
iii. Ugumu wa kupata taarifa halisi za mapato wanayolipwa wafanyakazi wataalamu kutoka nje ya nchi. Mathalan, katika miradi ya uwekezaji na hoteli, hali ambayo inasababisha kulipwa viwango vidogo au kutolipwa kabisa kwa kodi stahiki.
iv. Wafanyabiashara kutotumia mifumo ya kieletroniki katika shughuli zao za kibiashara, jambo ambalo linaathiri upatikanaji wa takwimu na ukusanyaji kodi kwa usahihi.
v. Kuwepo kwa biashara za magendo yanayofanyika baharini na nchi kavu jambo ambalo linapunguza mapato ya Taasisi zetu za Kodi hususan katika kisiwa cha Pemba.

vi. TRA kutokuwa na jengo kwa ajili ya Ofisi za kodi za ndani (TRA Domestic Revenues) katika Wilaya ya Wete - Mkoa wa Kaskazini Pemba.
vii. Kuwepo kwa utitiri wa kodi na tozo kwa mizigo inayopitishwa katika bandari za Pemba. Jambo hili husababisha wafanyabiashara kuwa na malamiko mengi na pia husababisha kupanda sana kwa bei za bidhaa mbali mbali hususan bidhaa za chakula ukilinganisha na Unguja.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kupitia TRA Zanzibar na ZRA kuendelea na juhudi za kutoa elimu na kuongeza uhamasishaji wa ulipaji wa kodi kwa wananchi ili kuinua mwamko wa kulipa kodi kwa hiari. Sambamba na hilo, Serikali haina budi kuhakikisha inadhibiti kwa kiasi kikubwa ubadhirifu wa fedha za umma ili kuwapa morali na hamu wananchi kulipa kodi kwa hiari.
ii. Kamati inaishauri Serikali kupitia Mamlaka zake za Mapato yaani Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kushirikiana na Mamlaka ya Mapato ya Kenya (KRA) kufanya makubaliano ya kuwezesha makontena ya mizigo ya wafanyabiashara kutoka Pemba yanayopitia katika Bandari ya Mombasa yanafunguliwa ili mizigo iliyomo katika makontena hayo iweze kusafirishwa na meli ndogo ndogo na majahazi. Jambo hili linahitaji makubaliano na mikakati ili kudhibiti upotevu wa mapato. Jambo hili litasaidia kupunguza msongomano wa meli za mizigo kusubiri muda mrefu ili kupata nafasi ya kufunga gati katika Bandari ya Malindi Zanzibar, hii itasaidia kupunguza gharama za usafirishaji wa mizigo inayoletwa Zanzibar.
iii. ZRA na TRA zianzishe vitengo vya Ukaguzi wa Kiuchunguzi (Forensic Audit) sambamba na kuvijengea uwezo kwa kuwapa mafunzo ya kutosha watendaji wake. Aidha, Serikali ihakikishe kunakuwepo na mashirikiano ya karibu kwa taasisi mbali mbali zinazohusika na wataalamu kutoka nje wanaokuja kufanya kazi nchini ili kubaini kwa haraka taarifa zao sahihi.
iv. ZRA na TRA ziweke mipango madhubuti ya kuwapitia wafanyabiashara mara kwa mara katika vituo vyao vya biashara ili kuwashajihisha kuongeza matumizi ya TEHAMA na kurahisisha ulipaji kodi na utunzaji wa kumbukumbu

za biashara zao.

v. Katika kudhibiti kadhia ya kuwepo biashara ya magendo Pemba, taasisi nyingi zimejikita katika kufanya doria mfano TRA – Pemba lakini Kamati inaishauri Serikali kupitia Kikosi cha Kudhibiti na Kuzuia Magendo (KMKM) kuweka mipango madhubuti ya kufanya doria katika maeneo ya visiwa vyetu. Kamati imebaini mara nyingi KMKM inashindwa kutekeleza majukumu hayo kwa kuwa vyombo vyake kukosa mafuta au kuzidiwa uwezo na vyombo vya wafanyabiashara za magendo. Aidha, KMKM ishirikiane na ZMA ili kubaini meli zilizopo katika ukanda wetu zenye viashiria ya kufanya magendo hususan magendo ya mafuta ya gari ambayo ndio hufanywa Zaidi katika kisiwa cha Pemba.

vi. TRA kukosa jengo Wete ni jambo ambalo linapunguza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, Kamati inaishauri Serikali kutafuta jengo haraka japo la kukodi kwa kuanzia sambamba na kuanza kutafuta jengo jengine au kushirikiana na taasisi nyengine ya Serikali.

vii. Kutokutozwa kodi au tozo kwa bidhaa zinazopelekwa Pemba ambazo zimeshatozwa kodi au tozo hizo pindi zilipoingia katika bandari ya Malindi kutoka nje ya nchi ili kuepusha bidhaa hizo kutozwa kodi au tozo hizo hizo mara mbili. Aidha, kwa zile kodi au tozo ambazo bado hazijalipwa, kuwekwe utaratibu wa ufanyaji wa malipo ya pamoja ili kuepusha utitiri wa kodi na tozo zinazopaswa kulipwa.

## MAMLAKA YA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPRA)

Mamlaka Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA) ina jukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli zote za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar. Udhibiti wa shughuli hizi unatekelezwa kupitia Programu kuu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu ambayo inajumuisha kuanzisha na kusimamia miongozo ya kitaalamu, kufanya ufuatiliaji wa kazi za utafutaji na uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia, kuzifanyia tathmini

kazi za utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia na usimamizi wa mazingira na utendaji kazi wa Mamlaka.

### Changamoto Zilizobainika

i. Mamlaka inakabiliwa na uhaba wa fedha za ruzuku ya matumizi mengineyo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao hali inayochangia pia kushindwa kutekeleza Mpango wa Mafunzo kwa watendaji wake.
ii. Kutoingizwa kwa fedha za maendeleo kunapelekea kuchelewa kuanza kwa Mradi wa Kituo cha Kudumu cha Uhifadhi wa Taarifa za Mafuta na Gesi (Data Center).

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kuipatia Mamlaka fedha za matumizi mengineyo kwa wakati ili Mamlaka iweze kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi. Shughuli zote zinazohusiana na utafutaji na uhifadhi wa taarifa za zoezi la utafutaji mafuta na gesi asilia zinapaswa kupewa kipaumbele.
ii. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha za mradi wa ujenzi wa Kituo cha Kudumu cha Uhifadhi wa Taarifa za Mafuta na Gesi zinapatiwa Mamlaka kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi ili kuwepo na uhifadhi mzuri wa taarifa hizo.

## KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA ZANZIBAR (ZPDC)

Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC) ni Kampuni iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 32 cha Sheria ya Mafuta na Gesi Nam. 6 ya 2016. Majukumu ya Kampuni ni kushiriki katika utafutaji na uchimbaji wa mafuta, kufanya biashara katika Sekta ya Mafuta na Gesi kwa niaba ya Serikali na kulinda maslahi ya Taifa katika biashara ya Mafuta.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kampuni kukosa chanzo cha mapato kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao.
ii. Kutokupatikana kwa wakati fedha za Ruzuku.
iii. Kukosekana kwa utaratibu wa uhakika wa kuhifadhi taarifa za mafuta na gesi.
iv. Gharama kubwa zinatumika katika ulipaji wa leseni ya matumizi ya “Kingdom

software" ambayo ni jumla ya TZS 24,606,560. Leseni hii ni kwa ajili ya kutafsiri taarifa za utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

v. Kumekuwepo na changamoto katika kutumia mfumo mpya wa manunuzi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kuisimamia Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta Zanzibar na kuhakikisha kuwa inaiandalia utaratibu wa uhakika wa kuhifadhi taarifa zinazopatikana za mafuta na gesi kwani kwa sasa taarifa hizo hazijahifadhiwa vizuri.

ii. Kamati inaishauri Kampuni kuwasiliana na Wakala wa Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ili kupata ufafanuzi wa namna ya kutumia mfumo wa manunuzi.

iii. Kamati inaisisitiza Serikali kuipatia Kampuni ya Mafuta fedha za ruzuku kwa wakati ili iweze kutekeleza wa majukumu yake kwa ufanisi.

## MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA (ZPPDA)

Kamati ilipokutana na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA) ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake iliyojumuisha mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbali mbali ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ili Mamlaka iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Mamlaka inakabiliwa na uhaba wa fedha za matumizi mengineyo hali inayoathiri utekelezaji wa majukumu na mipango ya Mamlaka.

ii. Kamati imebaini kuwa baadhi ya taasisi za Serikali ambazo zinatumia mfumo wa manunuzi zinakabiliwa na uelewa mdogo wa mfumo hali inayochangia kukwama kwa taratibu za manunuzi.

iii. Mfumo wa Manunuzi kwa njia ya kielektroniki kutounganishwa na mifumo mengine ya malipo kiasi ambacho kampuni zinazoshinda kutoweza kufanya malipo moja kwa moja ndani ya mfumo.

iv. Kukosekana kwa bajeti maalumu kwa ajili ya usimamizi wa mfumo wa

manunuzi katika utendaji wake.

v. Mamlaka inakabiliwa na uhaba wa watendaji katika shughuli zao. Kwa mfano katika kada ya wahandisi kuna muhandisi mmoja tu wakati mahitaji halisi ni wahandisi sita (6).
vi. Mamlaka kukosa jengo la kudumu kwa ajili ya Ofisi kwa Unguja na Pemba hali inayopelekea kutumia majengo ya kukodi kwa ofisi zake zote.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kutenga Bajeti maalumu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya usimamizi na matumizi mengine ya mfumo wa manunuzi.
ii. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mafunzo maalum ya mfumo wa manunuzi wa kielektroniki kwa watendaji wote wa taasisi za Serikali wanaohusika na kazi za manunuzi ili uweze kufahamika na kuweza kutumika ipasavyo.
iii. Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kuanza taratibu za kuipatia Mamlaka Fungu (Vote) ili kurahisisha upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa shughuli zake.
iv. Kamati inaishauri Afisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kupitia Kamisheni ya Utumishi wa Umma iandae kikao na Mamlaka ili kulitafutia ufumbuzi suala la maslahi ya watendaji wa Mamlaka. Kwa vile Muundo wa Utumishi wa Malaka umekemilika, Serikali haipaswi kuchelewesha maslahi ya watendaji hao.

### TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR (ZAHRI)

Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI) ilianzishwa kwa mujibu wa tamko la kisheria (legal Notice) Namba 25 ya tarehe 08 Januari 2018. Taasisi hii ina jukumu la kufanya tafiti na kugundua kitaalamu vyanzo vya maradhi mbali mbali na kuonesha majibu au matokeo ya tafiti hizo katika kuimarisha afya ya jamii.

### Changamoto Zilizobainika

i. Uingizwaji mdogo wa fedha katika ZAHRI unakwamisha utekelezaji wa majukumu hasa katika kazi za ufuatiliaji.
ii. Uhaba wa vyombo vya usafiri unarudisha nyuma utekelezaji wa majukumu ZAHRI hasa kazi za ufuatiliaji nje ya ofisi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuipatia ZAHRI fedha zake za mgao wa matumizi mengineo (OC) mara tu zinapoingia Wizarani. Kamati imebaini kuwa, kwa vipindi vitatu vya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2018/2019, 2019/2020 na 2020/2021 ZAHRI ilipatiwa mgao mdogo sana wa fedha ukilinganisha na bajeti iliyopangwa.
ii. Kamati inaishauri ZAHRI kuendeleza mashirikiano na taasisi nyengine zinazolingana kimajukumu ili waweze kupata kujifunza na uzoefu wa uendeshaji wa taasisi.
iii. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha ZAHRI inapatiwa fedha ili iweze kusaidia katika kutoa ushauri wa kitaalamu katika sekta ya afya nchini. ZAHRI ni taasisi muhimu sana ambayo inaweza kusaidia katika kudhibiti na kukinga maradhi mambo ambayo ni muhimu kuliko tiba. Tukiweza kukinga maradhi katika jamii maana yake tutaokoa fedha nyingi katika tiba na pia itawezesha nguvu kazi kutekeleza majukumu yake ya kujenga uchumi wa nchi.
iv. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha ZAHRI kupata misaada ya kifedha na uzoefu wa kazi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Wadhamini. Taasisi zinazofanya tafiti za afya duniani kote zimekuwa na nafasi kubwa ya kupata misaada na udhamini lakini kwa upande wetu inaonekana bado hatujachangamkia fursa au hatujaipa ZAHRI umuhimu inayostahiki.

**WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA ZANZIBAR (ZICTIA)**

Wakala wa Miundombinu ya Tehama Zanzibar (ZICTIA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria Nambari 15 ya mwaka 2020. Miongoni mwa majukumu

yake ni kusimamia na kuendesha Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano Zanzibar, Kusimamia kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa za Serikali pamoja na minara ya mawasiliano ya simu ili kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu bora ya mawasiliano iliyo salama na endelevu.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuharibika kwa Mkonga katika baadhi ya maeneo kulikotokana na utekelezaji wa miradi ya barabara ikiwemo barabara ya Kombeni - Kisakasaka.
ii. Kamati imebaini kuwa, baadhi ya maeneo ikiwemo eneo la SOS mkonga ulikatika. Aidha, katika eneo la Gamba hadi Matemwe nae neo la Tunguu – Suza, Kamati iliarifiwa kuwa, Mkonga uliharibiwa kutokana na kuliwa na panya na kuathiri utendaji kazi wake.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri ZICTIA kusimamia miundombinu ya Mkonga kwa kuhakikisha kuwa, taasisi nyengine zinafahamishwa maeneo yaliyopita mkonga ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza kutokana na utekelezaji wa miradi mengine.
ii. Kamati inazishauri Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na ZICTIA wakati wa kuweka miundombinu muhimu sana kama ya mkonga wa Taifa itekeleze kwa umakini mkubwa kwani fedha nyingi zimetumika. Mkonga (fiber optic cables) asili yake ni kigae ulipaswa kuwekwa kina cha kutosha chini ya ardhi na ulipaswa kuwekwa katika mabomba ya kuhifadhia (conduit pipes).

## KAMPUNI YA MWANI ZANZIBAR (ZASCO)

Kampuni ya Mwani Zanzibar (Zanzibar Seaweeds Company Limited - ZASCO) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Nambari 15 ya mwaka 2013. Kampuni hii ni kampuni inayojitegemea na inaendeshwa kutokana na hisa za wabia ambao Shirika la Bandari la Zanzibar (ZPC), Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC), Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF).

Lengo kuu la kuanzishwa Kampuni ya Mwani ni kuimarisha kilimo sambamba na soko la mwani ili kuwakomboa wananchi kutokana na umaskini na kuimarisha uchumi wa Zanzibar.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuwepo kwa uhaba wa wafanyakazi, vitendea kazi vikiwemo gari na maghala ya kuhifadhia mizigo na bidhaa za kampuni.
ii. Kuwepo kwa ushindani mkubwa wa makampuni mengine ya mwani.
iii. Mabadiliko ya tabianchi yanayopelekea athari katika kilimo cha mwani.
iv. Kukosekana kwa soko la uhakika kwa bidhaa zinazotokana na zao la mwani.
v. Kukosekana kwa mafunzo kwa wafanyakazi wa Kampuni ya Mwani
vi. Kuchelewa kwa Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Mwani.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kwa kuwa zao la mwani linategemewa na wananchi wengi na linaweza kutumika kuimarisha uchumi kwa wananchi, Kamati inaishauri Afisi ya Rais – Fedha na Mipango kuipa kipaumbele Kampuni ya Mwani kwa kuwaingizia fedha kwa wakati na kwa kiasi kinachohitajika. Kampuni hii bado ni changa ingawa ni muhimu sana, Serikali inapaswa kuhakikisha Kampuni inakuwa na kuweza kujitegemea kwa haraka.
ii. Kamati inaishauri Afisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuipa Kampuni kibali cha kuajiri watendaji wapya. Hali hii itasaidia kuongeza ufanisi wa ufanyaji kazi kwa Kampuni kutakapopelekea kuwa na uwezo kuimarisha zao la mwani.
iii. Licha ya Kampuni ya Mwani Zanzibar kufanikiwa kuongeza bei ya mwani kwa kununua mwani aina ya "Spinosum" kwa TZS 1,000 kutoka TZS 700 na mwani aina ya "Cottonii" kwa TZS 2,100 kutoka TZS 1,800, bado Kamati inaona bei hizi zipo chini mno na haziwezi kuimarisha uchumi wa wananchi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani ili kuongeza thamani na hatimae kuleta tija kwa wakulima wa zao hilo.
iv. Kamati inaishauri Kampuni, kufanya tafiti kuhusiana na changamoto

zinazokikabili kilimo cha mwani kutokana na mabadiliko ya tabianchi na pia kufanya tafiti kuhusu soko la mwani nje ya nchi.

## MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR

Kwa lengo la kufanikisha juhudi za kuimarisha afya za wananchi wa Zanzibar kwa kuhakikisha kwamba kila mtu anapata huduma za afya zilizo bora, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatekeleza hatua mbali mbali za uanzishwaji wa Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar.

Uimarishaji wa Sekta ya Afya na kuwezesha wananchi wote kupata huduma bora za afya ni jambo muhimu katika uchumi wa nchi yetu kwani kila mwananchi atakuwa na afya bora na kuweza kuchangia katika Pato la Taifa.

Ili kutekeleza shughuli mbali mbali uliyojiwekea, Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar umepanga kutumia jumla ya TZS 1,376,895,000 kutoka SMZ lakini mpaka kipindi cha nusu mwaka wa fedha (Julai - Disemba 2022/2023) kinamalizika hakukuwa na fedha iliyopatikana. Aidha, kwa upande wa fedha za Washirika wa Maendeleo, Mfuko umepata TZS 217,965,00 sawa na asilimia 100 ya lengo la nusu mwaka. Jambo hili linaipa wasi wasi Kamati juu ya utayari wa Serikali katika kuanzisha mfuko huu muhimu.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kukosekana kwa mchango wa fedha za SMZ zilizopangwa kutekeleza shughuli mbali mbali za Mfuko.
ii. Kutokupatikana kwa fedha za mgao wa matumizi mengineyo (OC) kunakopelekea Mfuko kutotekeleza majukumu yake.
iii. Kuchelewa kwa taratibu za manunuzi kunakopelekea kuchelewa kupatikana kwa wakati mifumo ya Mfuko ambayo ndiyo nguzo kuu ya uendeshaji wa Mfuko.
iv. Mfuko kukosa ofisi za kufanyia kazi hali inayopelekea watendaji kukosa ufanisi wa kazi.
v. Kukosekana kwa usafiri kunapelekea ugumu katika uratibu wa shughuli za

Mfuko.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaitanabahisha Serikali kwamba uimarishaji wa huduma za afya ni jambo muhimu sana. Serikali inapaswa kuupa kipaumbele Mfuko kwa kuingizia fedha kwa wakati ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma katika sekta ya afya.
ii. Kamati inaishauri Wizara ya Afya, kuratibu kwa haraka upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ya Mfuko.
iii. Kwa lengo la kurahisisha utaratibu wa manunuzi kwa Mfuko, Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuuwezesha Mfuko uwe na maafisa wake wa manunuzi ambao wataratibu shughuli zote za manunuzi za Mfuko badala ya kutumia watendaji wa Wizara.
iv. Kamati inashauri Serikali, iongeze juhudi ya kutafuta jengo kwa ajili ya Mfuko kutokana na umuhimu wake. Aidha, Serikali ijitahidi kuwatafutia usafiri kwani ni muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Mfuko.

## OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR (OCGS)

Kamati ya Bajeti ilitembelea Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar (OCGS) ili kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kwa mwaka 2021/2022. Miongoni mwa takwimu muhimu za kiuchumi ambazo zimekuwa zikikusanya na kuratibiwa Ofisi ya Mtakwimu wa Serikali ni Takwimu za Faharisi ya Bei ya Mlaji, Takwimu za Wageni Wanaoingia Nchini na Takwimu za Pato la Taifa.

Kamati imebaini kwa kiasi kikubwa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeweza kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio. Majukumu hayo ni kama vile; Uratibu wa Takwimu za Kiuchumi, Uratibu wa Takwimu za Kijamii, Kusimamia Viwango na Mifumo ya Kitakwimu, Matayarisho ya Sensa ya Watu na Makaazi 2022, Kufanya Uchambuzi wa taarifa za Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa mwaka 2020/21 na kutoa ripoti, Matayarisho ya Utekelezaji wa Mpango

Kabambe wa Takwimu, Tanzania wa Awamu ya Pili (Tanzania Statistical Master Plan – TSMP II) nakadhaalika.

### Changamoto Zilizobainika

i. Uhaba wa utaalamu wa uandaaji wa nyezo (tools) za kufanyia utafiti. Hii inatokana na kwamba kila tafiti inahitaji mbinu mpya za utafiti husika.
ii. Uhaba wa vitendea kazi za kitakwimu, mathaklan kukosekana gari kwa ajili ya kwenda kufanya kazi za nje ya ofisi (field works).

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Afisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuanza taratibu za kuajiri wataalamu wa kutosha wenye weledi ili kufanikisha ufanyaji wa tafiti kwa ufanisi. Sambamba hilo, Kamati inaishauri OCGS kuwapa mafunzo ya kutosha wataalamu waliopo. Katika dunia ya sasa mafunzo mengi ya kuongeza ujuzi yanaweza kufanyika kwa njia ya mtandao (online platform).
ii. Kwa lengo la kutatua changamoto ya usafiri, Kamati inaishauri Serikali kuitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto hii kwa kuhakikisha Ofisi ya Mtakwimu inapatiwa gari kwa mujibu wa mahitaji. Ifahamike kuwa, upatikanaji wa taarifa sahihi ndio nyenzo kuu ya kupanga mipango sahihi na inayotekelezeka.

### SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR

Shirika la Meli ni miongoni mwa mashirika ya umma ambayo yameanzishwa kwa lengo la kutoa huduma na hatimae kupata faida ili yaweze kutoa gawio kwa Serikali. Hata hivyo, Shirika hili kwa kipindi kirefu limekuwa likijiendesha kwa hasara hasa katika shughuli za uendeshaji wa meli ambapo kwa sasa Shirika halina meli inayofanya kazi.

Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilipitisha azimio la kuziuza meli tatu ambazo ni MV Maendeleo, MV Mapinduzi III na MT Ukombozi. Hatua hiyo ilifikiwa kwa ajili ya kulipunguzia mzigo wa gharama za uendeshaji Shirika.

Mbali na kuendesha meli za Serikali, Shirika hili ndio lenye jukumu la pekee Zanzibar la kutoa huduma za uwakala kwa meli zinazokuja katika bahari ya Zanzibar. Huduma za uwakala ni pamoja na kutaarifu taasisi zote husika juu ya ujio wa meli za kigeni, kufunga na kufungua makontena kwenye meli (Lashing and unlashing), ununuzi wa vipuri vya meli, kutoa huduma ya ulinzi kwa meli ikiwa imefunga gati, kusafirisha na kuwapokea mabaharia wa meli.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Shirika kuwa na meli moja tu inayofanya kazi ya MT Ukombozi II ambayo inaendeshwa kwa hasara.
ii. Shirika kujiendesha kwa mapato yanayotokana na shughuli za uwakala tu
iii. Ukosefu wa wahandisi wa meli wenye taaluma ya kisasa ya meli.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kupanga mikakati madhubuti itakayoweza kulihuisha Shirika badala ya kubaki kuwa wakala tu kwa meli za kigeni.
ii. Kamati inaishauri Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, kusimamia uendeshaji wa Shirika na kuzifanyia kazi changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa majukumu yake ili Shirika liweze kuleta ushindani katika sekta ya usafirishaji. Ni jambo linalofikirisha sana, kampuni ndogo na mpya za binafsi zinafanya vizuri katika uendeshaji wa meli zake lakini Shirika letu kongwe lenye uzoefu katika sekta ya usafirishaji baharini linaendeshwa kwa hasara kubwa.
iii. Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti wa namna bora ya uendeshaji wa meli hasa ukizingatia mapato hayaendani na matumizi ya kila siku.
iv. Kamati inaishauri Serikali kununua meli mpya ambazo zitaweza kufanya kazi kwa ufanisi katika mazingira yetu. Aidha, katika ununuzi wa meli hizo, Serikali iwashirikishe kwa karibu wataalamu ili zipatikane meli zenye uwezo na zitakazoweza kufanya kazi ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa muda mrefu.

**KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR (ZAFICO)**

Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) ipo chini ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Ilianzishwa Octoba, 2017 chini ya sheria ya usajili na uanzishwaji wa makampuni, Sheria namba 15 ya mwaka 2013. Kampuni hii ni kampuni inayoendeshwa kutokana na hisa za wabia ambao ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF - 45%), Shirika la Bima Zanzibar (ZIC - 10%), Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC - 18%) na Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC - 27%).

Lengo kuu la Kampuni ya Uvuvi ni kuimarisha sekta ya uvuvi kuwa endelevu na kufanya mabadiliko kutoka kuvua samaki kwa matumizi ya kawaida kwenda katika uvuvi kwa ajili ya matumizi ya biashara. Hata hivyo, lengo hili limekuwa gumu kufikiwa kwani Kampuni imenunua meli mbili za uvuvi lakini imeshindwa kuziendesha kutokana na ukosefu wa wataalamu wa kuziendesha meli hizo. Hali hii inaonesha kuwa manunuzi yalifanyika tu bila ya kuzingatia mpango kazi wa uendeshaji wa meli hizo.

Serikali yetu iliweka dhamira ya kuitumia vyema bahari inayotuzunguka kwa kuimarisha Uchumi wa Buluu (blue economy). Uchumi wa Buluu unafungamanishwa moja kwa moja na sekta ya uvuvi, ukulima wa mwani, uchimbaji wa mafuta na gesi, sekta ya utalii pamoja na shughuli mbali mbali zinazohusiana na matumizi bora ya rasilimali za bahari. Miongoni mwa maeneo ambayo bado hatujayatumia vyakutosha na linaweza kutuletea manufaa mengi zaidi ni eneo la uvuvi.

### Changamoto Zilizobainika

i. ZAFICO kushindwa kuzitumia meli mpya zilizonunuliwa kwa fedha za wananchi kwa lengo la kuvua katika bahari kuu.
ii. Kushindwa kutekeleza miradi kama ilivyopangwa kutokana na mwekezaji mwenza kushindwa kuingiza fedha kwa mujibu wa makubaliano ya mikataba.
iii. Kuwepo kwa ukosefu wa wataalamu wa kuendeleza Uvuvi wa Bahari kuu kama vile manahodha wa meli za uvuvi, mabaharia wa uvuvi na wahandisi katika meli za uvuvi na hivyo kushindwa kuzitumia meli na badala yake kuzikodisha meli hizo kwa mwekezaji wa ndani.

iv. Kukosekana kwa mazingira bora ya ufanyaji kazi na uhaba wa vitendea kazi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuweka mipango na mikakati madhubuti itakayosaidia Kampuni kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo suala la kuzitumia meli zilizonunuliwa kufanya uvuvi wa bahari kuu.
ii. Kamati inaishauri Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kufikiria kwa kina mpango wake wa kukodisha meli mpya za uvuvi kwa mwekezaji wa ndani. Kufanya hivyo, ni kuiondoa ZAFICO katika kazi yake ya msingi.
iii. Kamati inaishauri Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuiwezesha na kuisimamia Kampuni kwa ukaribu ili iweze kujiendesha kwa ufanisi na kupata faida hatimae kutoa gawio Serikalini.
iv. Kamati inaishauri Afisi ya Rais – Fedha na Mipango na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuweka mikakati ya pamoja ya kuhakikisha iweke mkazo katika Mradi ya Ujenzi wa Viwanda vya Kusarifu Samaki na Dagaa na Mradi ya Ujenzi wa Viwanda vya Kutengeneza Boti za Uvuvi inatekelezwa kwa haraka. Kiwanda cha Kusarifu Samaki na Dagaa kitasaidia kusarifu samaki na dagaa na kuwezesha kusafirisha nchi za nje. Zipo fursa kubwa za biashara ya samaki kwani kuna nchi nyingi ambazo hazina bahari. Aidha, Viwanda vya Kutengeneza Boti za Uvuvi vitasaidia kuzalisha boti hizo na kuwapatia wavuvi wadogo. Hatua hii itaokoa fedha nyingi za Serikali katika ununuzi wa boti za uvuvi.
v. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha shughuli za Uvuvi wa Bahari kuu kwa kuzitumia meli mpya kwani itasaidia katika kukuza mapato.

**SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR (ZPC)**

Miongoni mwa majukumu ya Shirika la Bandari la Zanzibar (ZPC) ni kutoa huduma za uingiaji na utoaji wa meli Bandarini (Pilotage), ufungaji na ufunguaji wa meli hizo gatini (Moorning/berthing), uangalizi wa alama za kuongozea usafiri wa bahari unaojumuisha minara na maboya (navigation aids), usimamizi wa

vyombo vya usafiri wa bahari kwenye maeneo ya Bandari. Kwa upande wa mizigo na shehena nyenginezo, Shirika lina wajibu wa kuihudumia mizigo hiyo kwa kazi za upakizi (loading), uteremshaji (discharging) na kuihifadhi (Warehousing) katika Bandari zake. Aidha, Shirika linafanya matengenezo ya vyombo vya usafiri wa bahari kwa kutumia Chelezo na Karakana yake Kuu ya Malindi (Unguja).

Kwa mwaka 2021/2022 iliidhinishiwa jumla ya TZS 32,245,948,236.18, hata hivyo Bodi ya Wakurugenzi iliridhia na kuidhinisha jumla ya fedha TZS 24,416,944,352.10 ambapo hadi kufikia mwishoni mwa mwaka Shirika limetumia jumla ya TZS 23,480,634,208.32 sawa na asilimia 96.17.

Katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka 2021/2022, Shirika limeidhinishiwa kutumia TZS 28,059,003,883.98, kwa ajili ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini, uimarishaji wa Bandari ya Mkoani, Ujenzi katika Bandari ya Mkokotoni, uimarishaji wa Bandari ya Malindi, Ununuzi wa Vitendea Kazi pamoja na Uimarishaji wa mifumo ya TEHAMA.

Katika kuimarisha utendaji kazi, Shirika la Bandari limenunua vitendea kazi vya kuhudumia mizigo vikiwemo Mizani 4, Mobile Habor Crane ya tani 124, Mobile Crane tani 60, Empty Reach Stacker, spreader 4, winch truck 1, Semi-trailer 1, Terminal tractor na trailer 1, mashine ya mobile habor crane ya tani 60 na Reach Stacker, ambapo jumla ya TZS 15,996,757,500.00 ziliidhinishwa kwa ununuzi wa vifaa hivyo. Baada ya kukamilika kwa taratibu za manunuzi ikiwemo kufungiana mikataba na kufanya malipo mbali mbali kwa manunuzi hayo, jumla ya TZS 15,943,932,461.00 sawa na asilimia 99.7 zimetumika kwa ajili ya malipo hayo.

Kwa upande wa mapato, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika lilikadiriwa kukusanya jumla ya TZS 42,317,368,347.54 na jumla ya TZS 44,006,895,565.86 zilikusanywa katika kipindi hicho ikiwa ni asilimia 104 ya makadirio.

Katika kutekeleza lengo la Shirika la Bandari la kuongeza ufanisi limeweka dhamira ya kutumia mifumo ya bandari ya kidijitali kwa kupanga kutekeleza

mradi wa utengenezaji wa Mfumo wa Kielekroniki wa Bandari (e-Port). Mradi wa huu utaharimu USD 6,569,143.31 ambazo ni zaidi TZS 15 bilioni bila ya kodi (VAT exclusive). Licha ya kwamba Mfumo huu utaweza kusaidia kuongeza mapato na kupunguza gharama za uendeshaji za Shirika lakini gharama za utengezaji wa mfumo huu ni kubwa sana.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Meli za mizigo kutoka nje kukaa nangani kwa muda mrefu zikisubiri kushusha makontena katika Bandari ya Malindi. Meli hizi zimekuwa zikisubiri kwa takriban siku 33 na hivyo kusababisha gharama za usafirishaji mizigo (freight) kupanda.

ii. Ukosefu wa eneo la kutosha la kuhifadhia makontena hali inayopelekea msongamano wa mizigo katika Bandari ya Malindi.

iii. Uhaba wa watendaji wataalamu.

iv. Uhaba wa vifaa vya kufanyia kazi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Serikali itekeleze kwa haraka mpango wa kuanzisha bandari kavu (ICD) sambamba na kuendelea na mipango ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa bandari mpya ya Mangapwani.

ii. Katika lengo la kutafuta ufumbuzi wa muda mfupi tukiwa katika mipango ya kutafuta ufumbuzi wa kudumu kuhusu changamoto ya meli za mizigo kusubiri muda mrefu, Kamati inaishauri Serikali ifanye utafiti wa kuchimba (dredging) katika bandari ya Mkoani Pemba ili iweze kuhimili meli zenye kina (draft) ya mita 11.

iii. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Shirika la Bandari Zanzibar ishirikiane na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) ili kufanya tathmini ya gharama za mradi wa utengenezaji wa Mfumo wa Kielekroniki wa Bandari (e-Port). Serikali inapaswa kujiridhisha, je gharama za kutengeneza mfumo huu ni sahihi yaani kuna thamani ya fedha? Je mfumo huu hauwezi kutengenezwa na wataalamu wa

ndani? Je teknolojia ya mfumo huu itaendana na mifumo mengine tuliyonayo? Je taarifa za Bandari zitakuwa salama?

## SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI ZANZIBAR

Shirika la Magazeti limeanzishwa kwa Sheria nambari 11 ya mwaka 2008. Shirika lina jukumu la kuchapisha magazeti ya kila siku yaani (Zanzibar leo), Magazeti ya kila wiki yaani (Zanzibar Mail na Zansport) pamoja na gazeti linalotolewa kila Jumapili na kusamabzwaZanzibar nzima pamoja na mikoa 22 ya Tanzania Bara.

Kwa kipindi cha Julai - Septemba , Shirika lilipanga kukusanya jumala ya TZS 212,400,000 milioni ambapo hadi kufikia Septemba 2022, Shirika lilikusanya jumla ya TZS 176,832,637.45 sawa na asilimia 83 ya makadirio. Makusanyo hayo yanajumuisha matangazo pamoja na mauzo ya magazeti.

Kwa upande wa matumizi, kwa kipindi cha Julai - Septemba 2022/2023, Shirika lilipanga kutumia TZS 270,392,806 sawa na asilimia 52 ya makadirio ya 521,850,000.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuwepo kwa changamoto katika mfumo wa manunuzi kunapelekea kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya majukumu.
ii. Shirika linakabiliwa na uhaba wa ruzuku kutoka Serikalini ambapo hadi kufikia Novemba 2022, kiasi kilichopatikana ni asilimia iliyopatikana ni 21 tu ya kilichopangwa.
iii. Kupanda kwa gharama za uchapaji magazeti hali inayopelekea Shirika kutumia kiasi kikubwa cha mapato yake kugharamia uchapishaji.
iv. Kuwepo kwa malimbikizo ya madeni kwa baadhi ya Taasisi za Serikali.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kuhakikisha taasisi zote zinazodaiwa na Shirika zinalipa madeni yao ili kuliwezesha Shirika kufanya kazi zake kwa ufanisi. Kuendelea kulimbikiza madeni kunahatarisha ustawi

wa Shirika letu.

ii. Katika kutanua wigo na uongezaji wa mapato, Kamati inalishauri Shirika kuongeza usambazaji katika mikoa ambayo haijafikiwa kwa kadri fursa za kibiashara zinapopatikana.

iii. Ili Shirika liweze kutekeleza majukumu yake kwa kujitegema, Kamati inaishauri Serikali kuwapatia mtambo wa uchapishaji.

iv. Kamati inalishauri Shirika kuratibu kikao na Mamlaka ya Ununuzi ili kupata mafunzo na msaada wa kutumia mfumo wa manunuzi.

## MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA)

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar Nam. 14 ya mwaka 2018. Jukumu la msingi la Mamlaka hii ni kutekeleza sera na sheria ya uwekezaji kikamilifu kwa nia ya kuwavutia wawekezaji wenye tija kwa manufaa ya nchi pamoja na wananchi wake.

Serikali kupitia Mamlaka imeweka nguvu katika Kuimarisha Maeneo Huru ya Uwekezaji yaliyopo Micheweni- Pemba.Dhamira ya Programu hii ni kuyafungua maeneo hayo kwa kuboresha miundombinu na kuyafanya maeneo hayo kwa lengo la kuwavutia Wawekezaji ili kuyafikia maeneo hayo kwa urahisi pamoja na kurahisisha huduma za kijamii. Eneo hilo lina jumla ya heka 808.8, eneo limejumuisha mradi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 13.5. Mradi huu ulisainiwa mnamo mwaka 2022 kati ya Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) pamoja na Wakala wa Barabara Zanzibar (ZANROADS) kwa gharama za TZS 6,989,145,000.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kamati imegundua kwamba, uchelewaji wa mpango mkuu (Master Plan) kufanyiwa kazi ni kutokana na uchache wa upatikanaji wa fedha za mradi.

ii. Pamoja na kuwa miundombinu ya barabara na umeme inayopatikana katika eneo hilo, Kamati imegundua kuwa miundombinu ya maji bado haijazingatiwa.

iii. Kuchelewa kwa Wakala wa Barabara (ZANROADS) kufanya taratibu za manunuzi kupitia mfumo ulioanzishwa kunapelekea uchelewaji wa mradi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kwa kuwa maeneo huru ni maeneo ya kimkakati kwa ajili ya uwekezaji katika kisiwa cha Pemba, Kamati inaishauri Serikali kuipa kipaumbele miradi inayotekelezwa kwa kuiingizia fedha kwa wakati na kwa mujibu wa mahitaji.
ii. Kamati inaishauri Mamlaka kuwapa kipaumbele wawekezaji wazawa pindi tu Mradi Kuimarisha Maeneo Huru ya Uwekezaji yaliyopo Micheweni utakapomalizika.

iii. Kamati inaishauri Wakala wa Barabara kuwa na mashirikiano na Mamlaka ya Ununuzi ili kupata uwelewa wa namna ya kuutumia Mfumo wa Manunuzi ili iweze kupata vifaa vinavyohitajika na kuweza kuukamilisha mradi wa barabara katika maeneo huru ya uwekezaji Micheweni.

### MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikina na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa pamoja zilianzisha Mfuko wa Maendeo ya Jamii (TASAF) mnamo mwaka 2000 ikiwa na lengo la kupunguza umasikini.

Kwa sasa Mfuko unaendelea na Awamu ya Tatu ya kipindi cha pili cha utekelezaji wa miradi yake ambapo unalenga kujumuisha kaya masikini. Usimamizi wa shughuli za TASAF Zanzibar unachangiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).
Utekelezaji kwa kipindi cha pili ulijikita katika utambuzi wa kaya masikini ambapo kwa upande wa Pemba shehia 51 ziliandikishwa na kupata kaya 14,957 ambazo kwa hatua ya awali zilifikia vigezo kati ya kaya 18,277.

Baada ya utambuzi wa kaya hizo, zoezi liliendelea la kukagua nyumba kwa nyumba (House to House Verification of Poor) na kugundua mambo mbali mbali kama vile; baadhi ya walengwa kujiandikisha katika shehia mbili mbili, baadhi ya kaya hazikuwa katika hali ya umasikini sana, baadhi ya wana kaya kutoonekana wakati wa ukaguzi na hatimae kutolewa kaya 2,525 ambazo zimekiuka taratibu.

Kamati ya Bajeti ilipofanya kazi na TASAF Pemba ilipata fursa ya kutembelea Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya kilichopo Shehia ya Kendwa - Pemba. Kupatikana kwa mafanikio katika mradi huu ni juhudi zilizochukuliwa na TASAF katika utowaji wa huduma za afya na kuleta maendeleo kwa wananchi wa maeneo ya karibu na eneo hilo. Kamati imefurahishwa na hatua hiyo na inaipongeza TASAF kwa mafanikio haya.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kamati imebaini kiwango wanacholipwa wananchi ni kidogo sana ukilinganisha na hali halisi ya maisha kwa sasa.

ii. Kutumika kigezo cha kuwa na nyumba kwa pande zote mbili, Tanzania bara na Visiwani hakiakisi uhalisia wa maisha ya walengwa.

iii. Kwa upande mwengine Kamati imebaini kuwa baadhi ya miradi inayogunduliwa na wana jamii haipewi kipaumbele.

iv. Kwa upande wa Kituo cha Afya Kendwa Pemba, Kamati imebaini kuwa Kituo cha Afya Kendwa kinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa gari ya kubebea wagonjwa, uhaba wa vyumba vya kulazia wagonjwa na na ukosefu wa huduma za upasuaji wa uzazi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri TASAF ifanye marekebisho ya vigezo vya kupima umaskini wa kaya. Kutokana na tofauti ya kimtazamo kuhusu umiliki wa nyumba kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara. Zanzibar unaweza kukuta kaya ni maskini kiasi ambacho inashindwa hata kumudu mlo kikawaida lakini

wanaweza kuwa na nyumba au banda la kuishi lakini kwa upande wa Tanzania Bara unaweza kuikuta kaya inamiliki kundi kubwa la ng'ombe lakini inaishi katika kibanda cha nyasi. Hivyo, kigezo cha kupima umaskini wa kaya hakiwezi kuwa nyumba kwa pande zote mbili Zanzibar na Tanzania Bara.

ii. Kamati inashauri ni vyema TASAF ikaweka mkakati wa kushajihisha kaya masikini kuandaa vikundi ili viweze kupewa mitaji itakayoweza kuwainua kiuchumi kuliko kupewa kiasi kidogo kwa mtu kaya mmoja.

iii. Kwa upande wa Kituo cha Afya Kendwa, Kamati inaishauri Wizara ya Afya kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa changamoto zinazokikabili Kituo cha Afya ili kukiwezesha kuhudumia vyema wananchi.

## SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR (ZIC)

Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) lilianzishwa mwaka 1969 likiwa ni miongoni mwa Mashirika yanayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100 na lipo chini ya Afisi ya Rais - Fedha na Mipango.

Shirika la Bima la Zanzibar ni miongoni mwa mashirika ya Serikali yameweza kupata faida na hatimae kuweza kutoa gawio kwa Serikali ambapo kwa mwaka 2021 Shirika limeweza kutoa gawio la TZS 500 milioni ikiwa TZS 400 milioni ni gawio kutokana na faida kwa mwaka 2020 na TZS 100 milioni ni bakaa la gawio kwa mwaka 2019.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kupitwa na wakati kwa Sheria ya Bima kifungu 3(3) kinachotoa adhabu ndogo ya kulipa Tzs 2000 kwa kosa la chombo kutembea barabarani bila ya Bima.
ii. Baadhi ya Taasisi za Serikali Zanzibar zinashindwa kulipia malipo ya bima kwa wakati licha ya kuwahi kuchukuwa ankara za malipo hayo na Taasisi nyengine za Serikali kutokatia kabisa kinga za bima za magari na mali zao.
iii. Shirika kukosa baadhi ya biashara kutoka katika Taasisi za Serikali kwa

upande wa Tanzania Bara.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inalishauri Shirika la Bima la Zanzibar kuendelea na mikakati ya kuliimarisha Shirika kwa kulitangaza zaidi Tanzania Bara ili liweze kuwa na wateja wa uhakika na kuleta ushindani kwenye Sekta ya Bima nchini.
ii. Kamati inalishauri Shirika lihakikishe linakamilisha na kuanza kutoa huduma ya Bima ya Kiislam "TAKAFUL" ili kuongeza mapato. Wapo wateja wengi wanaohitaji huduma ya bima lakini kutokana na imani zao za kidini hawakubaliani na bima ya kawaida. Hivyo, Bima ya Kiislam ni fursa nzuri ya kuongeza mapato.
iii. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha Miradi mikubwa ya Maendeleo inakatiwa Bima ili kuwa na kinga kwenye utekelezaji wake na vilevile kulisaidia Shirika kuongeza mapato.

# SEHEMU YA TANO

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA PROGRAMU MBALI MBALI

Katika kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023, Kamati ya Bajeti ilipokea na kujadili taarifa za utekelezaji katika baadhi ya Miradi ya Maendeleo Programu iliyomo katika Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023 sambamba na kufanya ziara katika maeneo ya miradi hiyo ili kutathmini kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo, thamani ya fedha inayotumika pamoja na kubaini changamoto zinazoibuka wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo. Miradi ya Maendeleo na Programu hizo iliyofanyiwa kazi na Kamati ni kama ifuatayo:

### MIRADI NA PROGRAMU ZILIZOTEKELEZWA KWA FEDHA ZA AHUENI YA UVIKO 19 KUTOKA SHIRIKA LA FEDHA DUNIANI (IMF)

Katika mwaka 2021 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepokea

mkopo nafuu wa dharura wenye thamani ya USD 571 milioni sawa na TZS 1.3 trilioni kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya kuhuisha uchumi baada ya athari za UVIKO 19. Kati ya fedha hizo, Zanzibar imepata USD 100 milioni sawa na TZS 230 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 17.8. Dhamira ya mkopo huu ni kuimarisha huduma za jamii, kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi na kuongeza vipato vya wananchi. Fedha hizi zimegawanywa katika sekta mbali mbali kama ifuatavyo:

**Sekta ya Elimu** ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 68.6 bilioni. Shughuli zilizotekelezwa kutokana na mgao huu wa fedha ni ujenzi wa madarasa mapya 104 na kuendeleza madarasa 247 yaliyoanzishwa kwa nguvu ya wananchi, ujenzi wa skuli 5 zikiwemo 3 za msingi na 2 za sekondari (Skuli 4 kati ya hizo ni za ghorofa), ujenzi wa vyoo 781 katika skuli mbali mbali, kufanya ukarabati katika skuli 10 (skuli 6 ukarabati mkubwa na zilizobaki ukarabati mdogo), kununua madeski 1,302 ya wanafunzi watatu watatu na kujenga nyumba 4 za walimu katika maeneo ya visiwa vidogo vidogo.

**Sekta ya Afya** ilipangiwa TZS 80.14 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Hospitali 10 za Wilaya, Hospitali 1 ya Mkoa wa Mjini Magharibi, ununuzi wa gari 12, ununuzi wa vifaa tiba, vifaa kwa ajili ya benki ya damu na matayarisho ya miradi.

**Sekta ya Uwezeshaji** ilipangiwa jumla ya TZS 81.87 bilioni kwa ajili ya kutekeleza miradi mikuu 5 kupitia taasisi mbali mbali kama ifuatavyo: Afisi ya Rais – Kazi, Uchumi na Uwekezaji imepangiwa jumla ya TZS 45.35 bilioni kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Mradi wa Kuwawezesha Vijana na Wanawake katika Ufugaji wa Nyuki.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imepangiwa jumla ya TZS 36.51 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi Kuimarisha Sekta ya Uvuvi ili kuongeza ajira.

Afisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imepangiwa jumla ya TZS 11.001 bilioni kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Ujenzi

wa Maeneo ya Kufanyia Biashara Unguja na Pemba.

Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilipata jumla ya TZS 406 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kuwawezesha Vijana Wanaoacha Dawa za Kulevya.

Hata hivyo, ukijumla fedha zote zilizotumika kwa kila taasisi na miradi husika unapata sawa na TZS 93.267 bilioni tofauti na kiasi cha fedha cha TZS 81.87 bilioni kilichoelezwa kutumika katika Sekta ya Uwezeshaji.

**Sekta ya Maji** ilipangiwa TZS 34.2 bilioni kwa ajili ya ujenzi wa matangi 10, uchimbaji wa visima 38, usambazaji bomba za maji, ujenzi wa vibanda vya kuendeshea pampu 52, magari mawili ya kuchimbia visima pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi.

**Sekta ya Nishati** ilipangiwa kutumia TZS 11.469 bilioni zilizowezesha Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kununua vifaa vya kusambazia umeme, ili kuhakikisha wananchi wa visiwa vya Zanzibar wanapata huduma muhimu ya uunganishaji wa umeme kwa bei nafuu. Miongoni mwa vifaa hivyo ni kama vile nguzo za kusambazia umeme mkubwa pamoja na nguzo za kusambazia umeme mdogo, vifaa vya uungaji umeme mkubwa na mdogo, waya wa kuunganishia umeme na mita za TUKUZA za njia moja.

**Shughuli za Uratibu** zilipangiwa jumla ya TZS 1,900,000,000. Fedha hizo zimetumika kama ifuatavyo:

Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani za Serikali waliingiziwa jumla ya TZS 95,000,000, fedha hizo ni kwa ajili ya kumlipa Mshauri Elekezi wa Ukaguzi wa Kitaalamu wa masuala ya ujenzi, vifaa vya ukaguzi, kuwajengea uwezo watendaji kuhusiana na ukaguzi wa majengo na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilipokea jumla ya TZS 73,554,950 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi (Kompyuta aina ya laptop 60 na desktop 10) kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iliingiziwa jumla ya TZS 200,000,000 kwa ajili ya kununulia jenereta na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilipata jumla ya TZS 406,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kuwawezesha Vijana Wanaoacha Dawa ya Kulevya. Mradi huu unawapatia vijana mafunzo ya amali katika ufugaji wa kuku, ng'ombe, ushoni, kilimo cha mboga mboga kwa kutumia 'green houses' na gereji katika Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia - Kidimni. Lengo la mradi huu ni kuwapatia elimu ya ujasiriamali vijana waliokubali kuachana na matumizi ya dawa za kulevya waliopo katika kituo hicho.

Tume ya Mipango ilipokea jumla ya TZS 1,209,710,000 bilioni kwa ajili ya shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini. Shughuli zilizofanyika ni ununuzi wa gari 5 kwa gharama ya TZS 598,000,000, ununuzi wa vitendea kazi (vikiwemo saver, printers, photocopy machines na computers) kwa gharama ya TZS 315,000,000, na jumla ya TZS 296,710,000 zimetumika kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji (ikiwemo ununuzi computers 22, printers 7, photocopy machines 4, stationaries, honda "click" 3 na kugharamia shughuli za usimamizi na ufuatiliaji). Maelezo ya jumla jumla ya matumizi ya fedha kama haya, hayaoneshi uwazi katika matumizi ya fedha za umma. Mathalan, ni vigumu kujua gharama ya kila kifaa ili kubaini thamani ya fedha iliyotumika.

Hata hivyo, ukijumla fedha zote fedha zote zilizotumika kwa kila taasisi shughuli za Uratibu unapata TZS 1,984,264,950 tofauti na kiasi cha fedha cha TZS 1,900,000,000 kilichopangwa kutumika katika Shughuli za Uratibu. Hii inafanya matumizi kuwa juu zaidi kwa TZS 84,264,950.

### Changamoto Zilizobainika

i. Baadhi ya miradi kupangiwa fedha zaidi ya mara moja. Mathalan, Mradi wa Kuwawezesha Vijana Wanaoacha Dawa ya Kulevya umepangiwa fedha katika fungu la fedha za Sekta ya Uwezeshaji na fungu la fedha za Shughuli za Uratibu. Jambo hili linaathiri hesabu ya jumla kuu na linatoa taswira ya kuwepo

kwa upotevu wa fedha za umma.

ii. Fedha nyingi zimetumika kwa ajili ya shughuli za kawaida za kiofisi kama vile kuwajengea uwezo watendaji na ununuzi wa stationaries, saver, printers, photocopy machines na computers, honda "click", jenereta na gari. Fedha za mikopo kama hizi za UVIKO 19 zilipaswa kutekeleza kazi za maendeleo tu na sio shughuli za kawaida ambazo zinawezekana kuzigharamia wenyewe.

iii. Kuwepo kwa mabadiliko mengi ya matumizi ya fedha katika maeneo mengi tofauti na ilivyopangwa awali. Jambo hili linafanya kuwepo kwa ugumu wa ufuatiliaji wa matumizi ya fedha husika.

iv. Kuongezeka kwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika maeneo mbali mbali ikiwemo Skuli ya Sekondari ya Pujini ambapo kati ya fedha zilizotengwa TZS 1.6 bilioni kulikuwa na ongezeko la TZS 460 milioni. Ongezeko hilo ni zaidi ya asilimia 15 inayohitajika kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi. Aidha, katika Skuli ya Kwale pia kumejitokeza ongezeko la fedha.

v. Fedha zilizoidhinishwa kupelekwa katika Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu hazikupelekwa na badala yake zimewekwa Benki ya CRDB na kuelekezwa ZAFICO kuzikopa na kuzitumia kununua boti za uvuvi. Jambo hili ni kinyume na taratibu za kibajeti. Matumizi yote yanapaswa kuidhinishwa na Katibu Mkuu kama ilivyoelekezwa na Baraza la Wawakilishi wakati wa kupitisha vifungu vya bajeti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

vi. Kukosekana kwa wataalamu wa Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kipindi chote cha ufungaji wa mifumo ya umeme katika majengo kunaweza kuleta ugumu wa kutambua tatizo pindi litakapojitokeza na kupelekea ugumu wa utatuzi wake.

vii. Kuongezeka kwa kazi kulipelekea kuzidi kwa muda wa utekelezaji mradi kwa baadhi ya maeneo kwa Unguja ikiwemo Hospitali ya Magogoni iliyoongezwa Wodi ya Watoto Njiti ambapo awali ilikuwa haipo katika mpango wa ujenzi wa hospitali hiyo. Aidha, kwa upande wa Pemba, Hospitali ya Wilaya ya Wete – Kinyasini, Hospitali ya Wilaya ya Micheweni na Hospitali ya Wilaya ya Chake Chake wakati Kamati ilipofanya ziara zilikuwa zipo nje ya muda uliopagwa.

viii. Kamati ilipofanya ziara katika Hospitali ya Wilaya ya Chake Chake – Vitongoji

ilibaini kuwa, katika utekelezaji wa mradi huo kumejitokeza changamoto ya kukosekana kwa vikao vya kufuatilia mradi huo (Site meetings).

ix. Kwa upande wa ZECO changamoto iliyobainika ni kuchelewa kufika kwa baadhi ya vifaa muhimu ikiwemo mita, nguzo za umeme kulikotokana na changamoto ya ushushaji wa mizigo katika bandari ya Malindi.

x. Katika ujenzi wa visima kwa baadhi ya maeneo ikiwemo Mkoa wa Kaskazini Pemba kumejitokeza tatizo la ardhi kutohimili ujenzi huo na kupelekea kujifukia kwa visima kabla ya kukamilika uchimbaji wake.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kutoa muhtasari wa uchambuzi na ufafanuzi wa fedha zilizotumika katika miradi na shughuli zote zilizotekelezwa kwa fedha za UVIKO 19 ili kujiridhisha matumizi yake na thamani ya fedha katika miradi na shughuli hizo. Aidha, katika ufafanuzi huo kuwepo na maelezo ya fedha zilizoripotiwa zaidi ya mara moja kwa shughuli au mradi moja.

ii. Kamati inaisisitiza Serikali kutotumia fedha za mikopo kwa ajili ya kazi za maendeleo tu. Haileti taswira nzuri kwa fedha za mikopo kutumika kwa ajili ya kugharamia shughuli za kawaida kama vile kuwajengea uwezo watendaji au kununua stationaries, kompyuta nakadhaalika. Jambo hili ni kinyume hata na agizo la Serikali wenyewe za kutaka taasisi zisitumie fedha za UVIKO 19 kwa kazi shughuli zisizo za maendeleo, hata mikataba ya Washauri Elekezi iliagizwa isainiwe na Afisi ya Rais – Fedha na Mipango.

iii. Kamati inaishauri Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuwataka wahandisi wa Wizara zao kushiriki kikamilifu katika ufungaji wa mifumo ikiwemo ya umeme na maji ili kupata uelewa mpana wa mifumo hiyo na kuweza kusaidia katika kufanya matengenezo iwapo kutajitokeza hitilafu zozote wakati wa matumizi ya majengo hayo.

iv. Kamati inaishauri Wizara ya Afya katika utekelezaji wa miradi yake kuhakikisha vikao baina ya Wizara na Kampuni inayotekeleza miradi vinafanyika kwa wakati ili kujadiliana kila hatua katika utekelezaji wa miradi pamoja na kutatua changamoto iwapo zitajitokeza.

v. Kamati inaishauri Serikali kusimamia taasisi zake katika utoaji wa zabuni kwa kuzipa Kampuni zenye uwezo katika utekelezaji wa miradi.
vi. Kamati inaishauri Serikali kupitia Tume ya Mipango kuhakikisha kuwa utekelezaji wa miradi unazingatia suala la kufanya upembuzi yakinifu kwa lengo la kujiridhisha utekelezaji wake pamoja na kukwepa mapungufu mbali mbali.
vii. Kamati inaishauri Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) wakati wa kutekeleza miradi yake kuandaa ratiba ambayo itazingatia masuala mbali mbali ikiwemo mabadiliko ya hali ya hewa ili kuepusha kasoro zinazoweza kujitokeza kutokana na kuanza utekelezaji wa mradi katika kipindi kilichokuwa si sahihi.
viii. Kamati inaishauri Serikali kurekebisha mfumo wa matumizi ya fedha za ununuzi wa boti ziwe chini ya Katibu Mkuu kama vile zilivyoidhinishwa katika Baraza la Wawakilishi.

## MRADI WA OFISI NA MAABARA YA TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS) - MARUHUBI

Baada ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Viwago Zanzibar (ZBS) chini ya Sheria namba 1 ya mwaka 2011, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda iliamua kuanzisha Mradi wa Ujenzi wa Ofisi na Maabara zinazoweza kufanya uchunguzi wa bidhaa mbalimbali kwa ajili ya kuthibitisha ubora na usalama wa bidhaa kabla ya kumfikia mtumiaji. Katika mwaka 2013 Taasisi ya Viwago kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilipitisha mchakato wa kumtafuta Mshauri Elekezi ambapo ilipatikana kampuni ya Mekon Arch Consult Limited ya Dar es Salaam na kukabidhiwa majukumu yake.

Mradi huu ni wa ujenzi wa ghorofa tatu (03) ambao umejengwa katika awamu mbili tofauti chini ya Mkandarasi World Class Engineering Contractor LTD (WCEC) ambapo awamu ya kwanza ilikua ni “structure” ya jengo na awamu ya pili ilikuwa ni “finishing” kwa ofisi na maabara. Mradi huu ambao unajengwa katika eneo la Maruhubi kupitia fedha za Maendeleo (Development Fund), unagharimu kiasi cha fedha TZS 5,200,367,918 pamoja na VAT kwa awamu zote mbili. Awamu ya

kwanza uligharimu TZS 1,345,565,802 na Awamu ya pili unatarajiwa kugharimu TZS 3,854,802,116. Taasisi ya Viwango ilichangia jumla ya shiliingi 200,896,787 kwa ajili ya mradi wa jengo la ofisi na maabara. Hadi Machi 2022 jumla ya TZS 2,765,048,528 zimelipwa.

Kukamilika kwa mradi huu, kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha mazingira ya utendaji kazi wa ZBS lakini mpaka sasa mradi huu umekwama katika umaliziaji wa malipo. Jengo limefunguliwa lakini imeshindikana mkandarasi kulikabidhi rasmi kwa ZBS.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuchelewa sana kwa malipo ya mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa jengo na ununuzi wa vifaa vya maabara.
ii. ZBS kutokufanya huduma ya udhibiti ubora, mfano simu, huduma kwa wateja (Customer care), usafirishaji nakadhaalika.
iii. Kutokutambulika kwa alama za kuthibitisha ubora za ZBS nje ya Tanzania. Mathalan, mfanyabiashara akienda hata katika nchi za Afrika Mashariki anapaswa kuwa na alama mbili yaani za ZBS na TBS.
iv. Kutokuwepo kwa utendaji kazi wa mashirikiano baina ya taasisi zinazofanya kazi bandarini licha ya kuanzishwa mfumo wa pamoja (one stop center).
v. ZBS wanakagua bidhaa zinazopita katika bandari rasmi tu, hivyo kufanya mizigo inayopita katika bandari bubu kutokukaguliwa ubora wake.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Afisi ya Rais – Fedha na Mipango pamoja na Taasisi ya Viwago Zanzibar (ZBS) ziweke kikao cha pamoja ili kutatua changamoto ya ucheweleshaji wa malipo ya mradi wa ZBS.
ii. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda iweke mikakati thabiti ya kuisaidia ZBS kufikia malengo ya udhibiti ubora katika huduma na sio kukagua bidhaa tu.
iii. Kamati inaishauri Serikali kuendeleza hatua za kuifanya ZBS kutambulika nje

ya Tanzania. Hatua hizi zinahitaji mikakati imara ya kuimarisha utendaji wa ZBS sambamba na kuingia mikataba ya mashirikiano na taasisi za kudhibiti ubora katika nchi washirika.

iv. Kamati inaishauri Serikali iratibu vikao baina ya taasisi zote zinazofanya kazi bandarini kama vile Mamlaka ya Bandari, ZBS, ZFDA, ZRA, TRA nakadhaalika ili kuweka mikakati ya kujenga utamaduni wa kufanya kazi kwa mashirikiano.

v. Kamati inaishauri Serikali iandae mpango wa kuiongezea nguvu kazi ZBS kwa kuajiri watendaji wapya ambao watasaidia kudhibiti bidhaa katika bandari bubu. Bidhaa zinazopitia bandari bubu haziathiri tu mapato yetu lakini pia zinaweza kuleta madhara makubwa kwa afya zetu.

## MRADI WA UJENZI WA MAREKEBISHO YA BANDARI YA MKOANI PEMBA PAMOJA MRADI WA UJENZI WA BANDARI YA SHUMBA

Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) lilipanga kuimarisha Bandari ya Mkoani kwa kufanyia marekebisho makubwa ikiwemo ujenzi wa eneo la kuhifadhia makontena, kutanua njia kwa ajili yakuwezesha vitendea kazi kupita kama vile Reach stacker,crane pamoja na Terminal tractor. Kujenga upya na kuongeza njia ya wapita kwa miguu yenye upana wa mita 1.5 na urefu wa mita 300. Kazi nyengine ni ununuzi wa vifaa vya kisasa vyenye uwezo wa kubeba kontena zenye uzito wa tani 60 na mobile crane yenye uwezo wa kubeba mizigo yenye tani 124.

Kazi zote hizi zinatekelezwa na Kampuni ya China Railway Bridge Engineering Compay kwa gharama za TZS 5,778,594,226.75, na mradi huu unatarajiwa kumalizika Novemba 2023.

Baada ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mweyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kufanya ziara katika bandari hiyo, alitoa maagizo ya kuongezwa kwa baadhi ya vipengele katika mradi huo ili kuweza kuleta tija kwa watumiaji. Katika kutekeleza maagizo hayo ya Mheshimiwa Rais ya kuongezewa kwa baadhi ya vipengele katika mradi, Shirika lilikubaliana na mkandarasi na

hatimae wakakubaliana na  gharama za mradi ziliongezeka na kufikia TZS 6,776,745,317.16 bilioni. Hadi kufikia Disemba jumla ya TZS 1,733,578,268.03 zimetumika sawa na asilimia 30 ya mkataba wa mwanzo kwa utekelezaji.

Kwa upande mwengine Kamati ilipokea taarifa ya Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Shumba ambapo Serikali iliamua kurasimisha Bandari hiyo kwa shughuli za kusafirishia mizigo pamoja na abiria ili kuondoa changamoto zinazowakabili wananchi wanaosafirisha mizigo baina ya Mombasa na Pemba.

Gharama za ujenzi huo ni TZS 5,772,880.00 nsa unatekelezwa na Kampuni ya Comfix Engeneering Smart Solution, mradi huu umeanza mwezi Juni 2022, na unatarajiwa kukamilika Octoba 2023. Hadi Kamati inapokea taarifa hii, Shirika limeingiziwa jumla ya TZS 1,761,752,068.60 sawa na asilimia 30 ya fedha zilizoizinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kamati imebaini uchelewaji wa upatikanaji wa fedha za miradi kutoka Serikalini kunapelekea kukwama kwa shughuli mbalimbali za utekelezaji wa miradi.

ii. Kutokufahamika kwa taratibu za mfumo wa manunuzi kwa baadhi ya watendaji wa Shirika, kunapelekea uchelewaji wa utekelezaji wa mradi.

iii. Kutokulipwa kwa fidia kwa wananchi walioathirika na ujenzi wa Bandari ya Shumba.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inalishauri Shirika, mbali na kufanya marekebisho ya ujenzi wa bandari upya pia ihakikishe bandari itafanya kazi kwa ufanisi pamoja na kuwa na wafanyazi wengi wenye weledi

ii. Kamati inashauri kuwa mifumo ya kielekteroniki itakayoanzishwa katika Bandari ya Malindi iweze kuunganishwa na Bandari za Pemba ili kuweza kuleta faida.

iii. Katika kufanikisha matumizi mazuri kwa ajili ya utekelezaji wa mradi, Kamati inaishauri Mamlaka ya Ununuzi kutoa mafunzo ya Mfumo wa Manunuzi kwa watendaji wa Shirika la Bandari ambao wanahusika na manunuzi ya Shirika.

## MRADI WA UIMARISHAJI ELIMU YA LAZIMA

Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima. Kupitia Mradi huu, Wizara ilipanga kukamilisha shughuli 5 zilizotengewa jumla ya TZS 11,265,000,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Mpaka kufikia Machi 2022, jumla ya TZS 5,427,797,522 sawa na asilimia 48.2 zilipatikana.

Shughuli za mradi ambazo zimetekelezwa kwa kipindi hicho ni Kuimarisha mazingira rafiki ya kujifunza na kufundishia katika skuli kwa kuzipatia skuli vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vya wanafunzi wenye mahitaji maalum, Kuwapatia walimu mafunzo ya mbinu za kufundishia hasa katika masomo ya hisabati, Sayansi na Kiingereza, Kuzipatia skuli Ruzuku ya Fedha kwa ajili ya gharama za uendeshaji, Kuzipatia zawadi skuli 300 zitakazofanya vizuri na kuonesha maendeleo katika mitihani ya Taifa ya darasa la Sita, Kidato cha Pili na kidato cha Nne, Kuandaa na kuimarisha matumizi ya TEHAMA na Media katika kujifunza (Virtual Learning Environment).

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuchelewa kuingiziwa fedha kutoka kwa baadhi ya wafadhili kutokana na athari za janga la UVIKO 19.
ii. Uhaba wa vifaa vya TEHAMA katika taasisi/skuli kunaathiri sana kasi ya maendeleo ya teknolojia katika kujifunza na hata kufundisha.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 tulikuwa tunakabiliwa na athari za za janga la UVIKO 19 lilipelekea Washirika wengi wa Maendeleo kutokuchangia

katika miradi. Kwa sasa hali imetengemaa, Kamati inaisisitiza Wizara, kufanya ufuatiliaji wa kina wa makubaliano ya michango ya Washirika wa Maendeleo na fedha zinapopatikana, ihakikishe miradi inatekelezwa kama ilivyopangwa.

ii. Suala la matumizi ya TEHAMA ni jambo la lazima kwa sasa ulimwenguni. Hivyo, Serikali iweke mkakati wa kipaumbele katika kuhakikisha vifaa vya TEHAMA vinapatikana katika taasisi/skuli zetu ili iwe rahisi kujifunza kupitia teknolojia za kisasa. Maarifa katika TEHAMA yatasaidia pia kufikia malengo yetu tuliyojiwekea katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 ya kuimarisha uchumi mtandao (digital economy).

## MRADI WA MPANGO WA UTAYARISHAJI WA MATUMIZI YA ARDHI ZANZIBAR

Mpango wa Utayarishaji wa Matumizi ya Ardhi ni jambo muhimu kwani huweka uwiano mzuri wa matumizi ya ardhi kwa kuzingatia idadi ya watu, ujenzi wa miundombinu endelevu, kilimo na uwekezaji. Zanzibar ilishawahi kufanya mipango mbalimbali ya Utayarishaji wa Matumizi ya Ardhi katika miaka ya nyuma. Mara ya mwisho Zanzibar kufanya mpango wa ardhi ni mwaka 1982.

Katika mwaka 2022/2023, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imepanga kutekeleza Mradi huu wa Mpango wa Utayarishaji wa Matumizi ya Ardhi kwa gharama TZS 1.0 bilioni.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuwepo kwa ujenzi holela na matumizi ya ardhi yasiyo rasmi ambayo hayaendani na ukuaji wa idadi ya watu nchini, na pia hayazingatii uendelevu wa miradi. Matumizi ya ardhi yasiyo rasmi huathiri kwa kiasi kikubwa mazingira ya nchi yetu.

ii. Kuwepo na migogoro mingi ya ardhi kutokana na kutokuanzishwa kwa mifumo ya kukabiliana na migogoro ya matumizi ya ardhi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kutokana na umuhimu wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali kuukamilisha mpango huo kwa wakati na kwa ufanisi.

## MRADI WA UJENZI WA NYUMBA NA MAHANGA YA KMKM KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 NA 2022/2023 KWA

## KAMANDI YA PEMBA

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) ni miongoni mwa Idara Maalum za SMZ kilichoanzishwa chini ya Sheria Nambari 1 ya mwaka 2003. Jukumu la msingi la Kikosi hichi ni kulinda usalama wa raia na maliasili za bahari kwa kuzuia njia zote zinazoweza kupitishwa magendo.

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kikosi kilipanga kutekeleza Miradi miwili (2) ya Maendeleo ya Ujenzi wa Afisi Kuu Wete na Ujenzi wa Hanga la Maaskari, Hospitali, nyumba ya Mkuu wa Kambi na nyumba ya walinzi (Quarter Guard) katika kambi ya Gando. Gharama za ujenzi huo ni TZS 2,435,313,050. Kati ya fedha hizo, TZS 1,760,004,850 ni kwa ajili ya ujenzi wa Afisi kuu Wete na TZS 675,308,200 ni kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Kambi ya Gando.

Kwa upande Mradi wa Ujenzi wa Afisi Kuu Wete, fedha zilizoingizwa ni TZS 811,002.425 sawa na asilimia 46 ya fedha zilizopangwa kwa ajili ya utekelezaji na hatua ya ujenzi huo umefikia asilimia 60. Aidha, kwa upande Mradi wa Ujenzi wa Kambi ya Gando kikosi kimeingiziwa jumla ya TZS 675,308,200 sawa na asilimia 100 ya fedha zote zilizopangwa kutumika. Mradi huu, umefikia hatua ya umalizaji (finishing).

Kamati ilipokuwa inafanya kazi zake za ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na kikosi cha KMKM, iliarifiwa kuwa, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Kikosi kilipanga kutumia jumla ya TZS 2,050,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 1,050,000,000 ni kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha uzamiaji na uwokozi na TZS 1,000,000,000 kwa ajilli ya ujenzi wa bwalo la Maafisa pamoja na nyumba za Maafisa katika kambi ya KMKM Wete. Hadi kufikia Disemba 2022, kwa kipindi hicho cha ufuatiliaji, Kikosi hiki hakikuingiziwa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kikosi kinakabiliwa na uchache wa wataalamu wa ujenzi hali inayopelekea kutumia wataalamu wa nje katika ujenzi wao.

ii. Uchelewaji wa upatikanaji wa fedha za miradi unapelekea uchelewaji wa miradi.

iii. Kutokupatikana kwa wakati kwa fedha za matumizi mengineyo (OC) kunapelekea kutokulipwa kwa wakati kwa wataalamu wanaopatikana nje ya Kikosi cha KMKM.

iv. Kamati imebaini hakukuwa na mashirikiano baina ya watendaji wa KMKM na Wakala wa Majengo wa Serikali (ZBA) katika utekelezaji wa mradi hali inayopelekea kukosa fursa ya kujua changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa mradi huo.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kurahisisha upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo ili kuweza kumalizika kwa wakati uliopangwa.

ii. Kamati inaishauri Serikali kusimamia suala la upatikanaji wa wataalamu wa ujenzi ili waweze kusaidia katika utekelezaji wa miradi ya Taasisi husika.

iii. Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa mashirikiano baina ya Wakala wa

Majengo (ZBA) na mafundi wa kikosi ili kuweza kujua changamoto katika utekelezaji na kuona namna gani ya kuweza kuzitatua kwa wakati ili kuweza kukamilisha miradi kwa wakati uliokusudiwa.

## MRADI WA UJENZI WA NYUMBA NA MAHANGA YA KVZ KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 NA 2022/2023

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kikosi cha Valantia (KVZ) kilipanga kutekeleza programu ndogo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kujenga Ofisi, nyumba na mahanga ya kulalia askari katika kambi zake za Pujini na Micheweni kwa upande wa Pemba na Kikungwi kwa upande wa Unguja.

Jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo ni TZS 1,500,000,000. Kamati ilipotembelea kikosi hicho Januari 2023, iliarifiwa kuwa hadi kufikia Juni, 2021 kikosi kiliingiziwa jumla ya TZS 300,000,000 ambapo kilijenga Hanga la kulala askari katika kambi ya Pujini.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kikosi cha Valantia kimepanga kuendelea na ujenzi wake kwa upande wa Unguja kwa kujenda kituo cha kuuzia mafuta katika kambi ya Muyuni, Hanga moja katika kambi ya Kikungwi. Ofisi na Hanga katika kambi ya Kiashange, ukarabati wa mahanga katika kambi ya Pangatupu, Hanga moja katika kambi ya Micheweni Ofisi katika kambi ya Pujini na kituo cha afya katika kambi ya Ndugukitu kwa upande wa Pemba lakini hadi Kamati inapokea taarifa hii Januari 2023, kikosi bado hakikuingiziwa fedha za utekelezaji wa mradi huo.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kukosekana kwa fedha kutoka Serikalini kumekwamisha uendelezaji wa miradi hiyo.

ii. Mchakato wa wazabuni kuchukua muda mrefu kutokana na mfumo wa manunuzi unaotumika sasa hali inayopelekea kuchelewa kukamilika kwa

miradi kwa muda uliopangiwa.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi zinapatikana kwa wakati

ii. Ili kuondokana na changamoto katika utumiaji wa mfumo wa manunuzi kwa baadhi ya vipengele, Kamati inaishauri Mamlaka ya Ununuzi kutoa elimu kwa watendaji wanaohusika na shughuli za manunuzi ya moja kwa moja na mfumo huo.

## MIRADI YA TUME YA MIPANGO ZANIBAR

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Tume ya Mipango Zanzibar imejipangia kutekeleza miradi minne (4) kama ifuatavyo:

### Mradi wa Usimamizi wa Upembuzi Yakinifu kwa Programu na Miradi ya Maendeleo

Lengo la mradi huu ni kuimarisha uandaaji na utayarishaji wa Ripoti za Upembuzi Yakinifu kwa Programu na Miradi ya Maendeleo. Mradi huu umebuniwa kutekelezwa baada ya kuonekana kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa Ripoti za Upembuzi Yakinifu kwa miradi mbali mbali. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mradi umepangiwa TZS 6.9 bilioni kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu kwa Programu/miradi ya maendele, kuandaa mfumo wa ukusanyaji taarifa na ripoti za upembuzi yakinifu kwa programu/miradi ya maendeleo pamoja na kujenga uwezo wa Taasisi na watendaji juu ya utayarishaji na uchambuzi wa ripoti za upembuzi yakinifu kwa programu na miradi ya maendeleo.

Kwa kipindi cha Julai – Septemba 2022, matayarisho ya utekelezaji wa mradi

ulianza na Sekta za Uchumi wa Buluu, Uvuvi, Mambo ya Kale, Ujenzi, Mawasiliano, Maji, Nishati na Madini ambazo zinaendelea kutayarisha Maandiko ya Awali (Concept Notes) juu ya miradi itakayoandaliwa Upembuzi Yakinifu.

**Mradi wa Kuimarisha Usimamizi, Kujenga Uwezo na Kuoanisha Mipango ya Kisekta, Kitaifa na Kimataifa**

Mradi huu una lengo la kuimarisha usimamizi na kuoanisha mipango ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (Zanzibar Development Vision 2050), Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP), Ajenda ya Afrika Mashariki (EAC Agenda 2050), Malengo ya Maendeleo ya Afrika (African Agenda 2063) pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Mradi umeanza mwaka 2022/2023 na umepangiwa TZS 530 milioni (TZS 300 milioni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na TZS 230 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Programu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

Mradi una lengo la kuwakwamua wananchi na umasikini kupitia urasimishaji wa ardhi na biashara ili ziweze kutumika katika juhudi za kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka 2022/23, Programu hii imepangwa kutumia kiasi cha TZS 4.5 bilioni (TZS 4.0 bilioni kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na TZS 500 milioni kutoka kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

**Mradi wa Uratibu wa Shughuli za Kupambana na Umasikini umeanzishwa**

Lengo la mradi ni kusaidia Serikali katika jitihada zake za kupunguza umasikini Zanzibar. Kwa kipindi cha mwezi wa Julai hadi Septemba 2022, Tume imefanya vikao vitano (5) na wadau wa Maendeleo wakiwemo Mashirika ya Maendeleo, NGOs na Taasisi za Serikali kujadili uratibu wa shughuli za Maadhimisho ya Wiki ya kupambana na Umasikini

### Changamoto Zilizobainika

i. Kamati imebaini kuwa, hakuna fedha zilizopatikana kwenye kipindi cha Julai hadi Septemba 2022/2023 kwa ajili ya miradi hiyo na baadhi ya shughuli zimefanyika bila ya fedha.
ii. Licha ya kuwa Tume ina Mradi wa Uratibu wa Pembuzi Yakinifu bado kuna taasisi zinatekeleza miradi husika bila ya kukamilika kwa Pembuzi Yakinifu.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali, kuweka utaratibu wa kufanya Upembuzi Yakinifu mwaka mmoja kabla ya mradi kutekelezwa ili kuwezesha kupanga bajeti sahihi ya utekelezaji wa mradi husika na kuondoa uchelewaji katika kutekelezwa miradi husika.
ii. Kamati inaishauri Tume ya Mipango kuratibu vyema upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hususan fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwa miradi mbali mbali ya maendeleo ili miradi hiyo iweze kutekelezwa kwa ufanisi.

### PROGRAMU YA UMWAGILIAJI MAJI KWA MWAKA 2021/2022 NA 2022/2023

Progaramu ya Umwagiliaji Maji inatekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa Mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 50 kutoka Benki ya Exim Korea. Kati ya fedha hizo, Dola 45.63 milioni ni kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji na Dola 4.32 milioni ni kwa ajili ya malipo ya Mshauri Elekezi kwa kusanifu, kutengeneza makabrasha ya zabuni na kusimamia ujenzi wa miundombinu.

Mkataba wa ujenzi wa mradi ulitiwa saini tarehe 06/12/2018 baina ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na Kampuni ya Ujenzi ya KOLON – HANSOL JV kutoka Korea. Jumla ya hekta 1,053 katika mabonde ya Kibokwa, Chaani, Kinyasini, Kilombero, Cheju A kwa Unguja na Pemba bonde la Mlemele yametekelezwa katika mradi.

## Changamoto Zilizobainika

i. Kutokufanikiwa kwa baadhi ya miundombinu ya umwagiliaji iliyojengwa na kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Katika bonde la Kinyasini halikusanyi maji ya kutosha. Aidha, bwawa la Chaani linavujisha maji hali inayopelekea kufanyiwa tena marekebisho kwa bwawa hilo.
ii. Wakulima kushindwa kuyatumia maeneo yao kwa kipindi kirefu kumechangia katika kupunguza uendelezaji wa shughuli za kilimo katika maeneo hayo na kupunguza vipato vyao.
iii. Kamati imebaini kuwa, tafiti (studies) zilizotumika katika utekelezaji wa mradi wa umwagiliaji zilikuwa za kipindi cha nyuma kiasi ambacho tayari kumeshajitokeza mabadiliko mengi katika eneo hilo.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Wizara kuzitafutia ufumbuzi changamoto ya kutokusanyika maji katika bonde la Kinyasini pamoja na kuvuja kwa bwawa la Chaani ili utatuzi wake usaidie katika kufikia lengo lililokusudiwa katika mradi huo.
ii. Katika utekelezaji wa miradi, Kamati inaishauri Wizara kutumia muda wa kutosha katika kutafakari maeneo ya utekelezaji wa miradi hiyo ili watendaji waweze kufanya maamuzi sahihi kwa kila hatua ya utekelezaji.

## PROGRAMU YA UJENZI WA BARABARA ZA NDANI NA MATENGENEZO YA BARABARA MJINI

Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani pamoja na Matengenezo ya Barabara za Mjini kwa mwaka wa 2022/2023, barabara za ndani zilizopangwa kuendelezwa zina urefu wa kilomita 275.9 Unguja na Pemba na barabara za Mjini urefu wa kilomita 100.9. Programu hii kumepangwa kuendelezwa barabara kuu nne Unguja na Pemba ambazo ni Barabara za Wete – Chake, Barabara ya Mkoani – Chake, Barabara ya Tunguu- Makunduchi na Barabara ya Fumba – Kisauni.

Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Ndani ulipangiwa kutukia jumla ya TZS 30 bilioni na Mradi wa Barabara za Mjini Unguja

ulipangiwa TZS 135.6 bilioni. Fedha hizo ni kwa ajili ya kazi ya ujenzi, malipo ya fidia na gharama za msimamizi wa ujenzi.

### Changamoto Zilizobainika

i. Upatikanaji mdogo wa fedha za mradi kutoka Serikalini. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Ndani ulipangiwa TZS 30,000,000 na hadi kufikia Disemba 2022, jumla ya TZS 4,400,663,341.58 zimepatikana sawa na asilimia 15% ya makadirio ya bajeti.
ii. Kampuni ya ASSER ya Uturuki wakati ilipoanza kazi ililazimika kukodi vifaa kutoka Tanzania Bara kutokana na vifaa vya Kampuni hiyo kuwa nje ya nchi na kulikuwa na ugumu wa kuvisafirisha.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuja na mkakati mpya wa kugharamia miradi ya barabara kwa kutumia mfumo wa EPC + Finance. Katika mfumo huu, barabara zinatengenezwa kwa mikopo baadae Serikali italipa taratibu badala ya kutumia utaratibu wa awali wa kujenga kwa fedha za ndani hali inayopelekea miradi ya ujenzi wa barabara kutekelezwa kwa kasi ndogo mno. Pamoja na kuanzisha mfumo katika utekelezaji wa miradi ya barabara, Kamati inaishauri, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuongeza umakini katika kusimamia miradi hiyo.
ii. Mkataba wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Ndani ulipaswa kufuata utaratibu wa mfumo wa EPC + Finance. Kwa utaratibu huu mkandarasi alitakiwa kutumia fedha zake kulipia gharama za ujenzi lakini katika mkataba huu kuna kipengele cha kulipwa gharama za awali (advance payment) ya USD 8 milioni. Kamati inaishauri Serikali inapoingia mikataba ya EPC + Finance ihakikishe inafata taratibu za mikataba hii na kuepuka fedha za awali.
iii. Kamati inaishauri Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, kuhakikisha kuwa barabara zinazotengenezwa zinawekwa misingi ya kupita maji ili zisiharibike kinapokuja kipindi cha mvua. Barabara nyingi hazidumu kwa sababu ya kutuama maji ya mvua.

iv. Kamati inaishauri Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi pindi inapoingia makubaliano na wakandarasi katika utekelezaji wa miradi yake, kuhakikisha inajiridhisha na uwezo wa wakandarasi hao kwa maeneo tofauti ikiwemo uwezo wa kifedha, vifaa na utaalamu wa kutekeleza kazi husika.

## PROGRAMU YA KUIMARISHA MAENEO YA KIHISTORIA KWA MWAKA WA FEDHA 2022

Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria ilianza mwaka 2017/2018 na inatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2024/2025. Jumla ya fedha zilizotengwa kutekeleza Programu hii ni TZS 7.50 bilioni kutoka Serikalini.

Katika Programu hii, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imepanga kutekeleza miradi mwili ambayo ni Mradi wa Kuimarisha Eneo la Chwaka Tumbe na Mradi wa Kuimarisha Pango la Kijiji na Pango la Watoro.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilipata fursa ya kutembelea eneo la kihistoria la Chwaka Tumbe na kuona utekelezaji wake. Mradi huu ulipangiwa jumla ya TZS 738,212,100.00/= ambapo Mjenzi wa mradi huu ni **Osaju Company Limited.** Kwa kipindi hicho cha ufuatiliaji, Kamati iliarifiwa kuwa tayari Kampuni imeshalipwa jumla ya TZS 654,236,419.09/= sawa na asilimia 89 ya fedha zilizopangwa na hatua ya utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 90.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kamati imebaini kwamba Wizara ya Utalii kwa upande wa Pemba inakabiliwa na uhaba wa Ofisi pamoja na uchakavu wa jengo hali inayopelekea ufanisi mdogo katika kutekeleza majukumu yake.

ii. Wananchi kuvamia baadhi ya maeneo ya kihistoria yaliyopo Pemba kwa shughuli za kilimo na ufugaji hali ambayo inazorotesha hatua za maendeleo.

iii. Kukosekana kwa hati miliki katika baadhi ya maeneo ya Kihistoria yakiwemo Mkamandume, Ole na Chwaka Tumbe.

iv. Uchakavu wa miundombinu ya kuweza kufikia sehemu za kihistoria.

v. Uchelewaji wa uingiaji wa fedha za miradi hali inayopelekea kusuasua kwa utekelezaji wa miradi hiyo.

vi. Afisi kuu Pemba pia inakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi wakiwemo walinzi hali inayochangia kwa baadhi ya maeneo ya kihistoria kuvamiwa.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuchukua jitihada za kuwatafutia Ofisi watendaji wa Wizara hii Pemba.

ii. Kamati inaishauri Wizara kufuatilia upatikanaji wa walinzi ili kuweza kuwadhibiti wavamizi.

iii. Kamati inaishauri Wizara kufuatilia upatikanaji wa hati miliki ili kurahisisha utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa katika maeneo hayo.

iv. Kamati inaishauri Wizara kuimarisha miundombinu ya barabara za kelekea katika maeneo ya Kihistoria.

v. Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kuwapatia fedha Wizara husika kwa mujibu wa bajeti waliyoipanga ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli zake.

vi. Kwakuwa Utalii ni sekta muhimu ambayo inachangia sehemu kubwa katika Pato Taifa letu, Kamati inaishauri Serikali kuipa kipaumbele miradi hii ili kuweza kuwavutia watalii.

## PROGRAMU YA KUIMARISHA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ikishirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kupitia Programu ya Uimairishaji wa Viwanja vya Ndege kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imepanga kutekeleza miradi miwili. Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi ulipangiwa kutumia TZS 6,600,000,000 na Mradi wa Uimarshaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba ulipangiwa kutumia

TZS 8,000,000,000.

Katika kipindi cha Julai – Septemba 2022, Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi ulipangiwa kutumia TZS 1,160,000,000 kwa ajili ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Uwanja, hata hivyo hakuna fedha iliyopatikana kwa kipindi hicho.

Kwa upande wa Mradi wa Uimarshaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba hadi kufikia Oktoba 2022 Serikali ilikuwa katika hatua ya mazungumzo na Kampuni ya PROPAV ya Hispania kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja huo. Ujenzi huo unategemewa kuanza rasmi mara tu taratibu za fedha zitakapokamilika.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Programu ya Uimarishaji wa Viwanja vya Ndege vya Nungwi na Pemba.

ii. Kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa Kigunda bila ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kukamilisha upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa shughuli za mradi ili kuepusha hasara kwa Serikali.

ii. Kamati inaishauri Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kujenga uzio kwenye kiwanja cha ndege Nungwi ili kuepusha uharibifu wa miundombinu.

iii. Kamati inaishauri Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wakati wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege kuhakikisha inatafuta Mshauri Elekezi mwenye uzoefu, uwezo, na uweledi kwenye ujenzi wa viwanja vya ndege.

iv. Kwa upande wa kiwanja cha ndege Pemba Kamati inaishauri Serikali kulipa fidia haraka iwezekanavyo kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa uwanja huo.

## PROGRAMU YA UJENZI WA BARABARA KUU KWA BARABARA YA CHAKE CHAKE - WETE NA CHAKE CHAKE - MKOANI

Programu hii inajumuisha Mradi ya Ujenzi wa Barabara Kuu ya Chake - Wete yenye urefu wa kilomita 22.1 na Mradi ya Ujenzi wa Barabara ya Chake - Mkoani yenye urefu wa kilomita 43.5 kwa mwaka fedha 2022/2023.

Barabara ya Chake-Wete inajengwa na Kampuni ya MECCO chini ya mshauri elekezi Dar al Handasah kwa ufadhili wa BADEA, SAUDI FUND na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo itagharimu jumla ya TZS 23.6 bilioni kwa ajili ya ujenzi na USD 1,076,100 kwa ajili ya malipo ya mshauri elekezi. Hadi kufikia mwezi wa Oktoba, 2022 hatua ya ujenzi iliyofikiwa ni usafishaji wa barabara kwa urefu wa kilomita 10.7 na kutengeneza tuta la barabara pamoja na uwekaji kifusi katika tabaka la mwanzo la barabara kwa urefu wa kilomita 3.5. Aidha fidia kwa wananchi 139 zimelipwa kwa eneo la barabara lenye urefu wa kilomita 4.5 ambapo jumla ya TZS 1.76 bilioni zimetumika.

Kwa upande wa barabara ya Chake-Mkoani hadi kufikia Septemba 2022 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilisaini mkataba wa ujenzi na Kampuni ya PROPAV na MECCO. PROPAV ndio mfadhili wa barabara ya Mkoani-Chake na ameingia ubia na MECCO.

### Changamoto Zilizobainika

i. Mkandarasi amekuwa na uhaba wa vifaa vya ujenzi kwa barabara ya Chake-Wete jambo ambalo linazorotesha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara hiyo.
ii. Kuchelewa kwa malipo ya fidia za majengo na miti ambayo inapelekea mkandarasi kutofanya kazi kwa mpangilio unaotakiwa katika mradi wa Barabara ya Chake – Wete.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Ili kutatua changamoto ya uhaba wa vifaa kwa wakandarasi wa barabara, Kamati inaishauri Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha

inasimamia agizo lililotolewa kwa mkandarasi juu ya uletaji wa vifaa vya kutosha ili kuepusha uzoroteshaji wa mradi huo.

ii. Kamati inashauri malipo ya fidia kwa wananchi walioathirika na ujenzi wa barabara ya Chake-Wete kulipwa haraka iwezekanavyo. Aidha kwa upande wa barabara ya Chake-Mkoani tathmini ifanywe na mthamini mkuu wa Serikali kwa haraka ili ujenzi wake utakapoanza mwezi Machi 2023 wananchi waweze kulipwa fidia zao kwa wakati.

iii. Kamati inaishauri Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha ujenzi wa barabara zote unakamilika kwa muda uliopangwa ili kuepusha Serikali kuingia katika gharama zisizo za lazima.

## SEHEMU YA SITA

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Kwa lengo la kubaini ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na bajeti za Serikali za Mitaa hususan katika utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali, Mradi wa Ujenzi wa Stendi za Magari na Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Daladala. Kamati ilizitembelea Halmashauri, Mabaraza ya Miji na Manispaa zote kwa Unguja na Pemba. Tathmini ya Kamati kwa Halmashauri, Mabaraza ya Miji na Manispaa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

### HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI

#### Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imetekeleza Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamalikatika eneo la Tumbe kupitia fedha za ahueni ya UVIKO 19 ambapo Mshauri Elekezi alikuwa ni Wakala wa Majengo Zanzibar na Mkandarasi alikuwa ni Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM). Jumla ya TZS 1,033,343,935 zilisainiwa kwenye mkataba na ndio zimetumika. Kituo hicho kimeshakamilia kwa asilimia 100. Kwa upande mwengine jumla ya TZS 567,333,525 zimeongezwa kwa ajili ya ujenzi wa ukuta, uwekaji wa taa za umeme wa jua (solar) na uandaaji wa eneo (landscaping) lakini zilikuwa bado hazijapatikana.

#### Mradi wa Ujenzi wa Stendi za Gari ya Kinowe Konde

Mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Gari katika eneo la Kinowe Konde ulitengewa TZS

250 milioni kwa mwaka 2022/2023 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni na kwa upande wa Afisi ya Raisi Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ilichangia jumla ya TZS 600 milioni. Halmashauri ilifunga mkataba wa TZS 1,046,224,500 na kampuni ya Comfix & Engineering Co. Ltd mwezi Mei 2022. Hadi kufikia Oktoba 2022 jumla ya TZS 619,725,290 zimeshatumika.

**Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Daladala**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilitenga jumla ya TZS 20,000,000 kutekeleza mradi wa vituo vya daladala katika maeneo ya Wingwi mapofu, Kilindini, Tumbe na Kizota. Kampuni ya Micheweni Engineering Contractor Partnership ilifanikiwa kufunga mkataba kujenga vituo hivyo. Hadi kufikia Oktoba 2022 ujenzi ulikuwa unaendelea na malipo ya TZS 10,000,000 yalifanyika.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Fedha za ahueni ya UVIKO 19 kwa ajili ya ujenzi wa maeneo ya wajasiriamali hazikuhusisha gharama za kumlipa Mshauri Elekezi ambae ni Wakala wa Majengo Zanzibar.
ii. Hakukuwa na Upembuzi Yakinifu uliofanyika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.
iii. Kutopatikana kwa fedha za ujenzi wa ukuta, uwekaji wa taa za umeme wa jua (solar) na uandaaji wa eneo (landscaping) kwenye eneo maalum la wajasiriamali Tumbe.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo gharama za malipo ya Mshauri Elekezi zitengwe ili kuwezesha kupatikana kwa Mshauri Elekezi kwa utaratibu uliopangwa.
ii. Kamati inashauri kuengezwa kwa eneo la maegesho na maduka katika mradi wa ujenzi wa kituo cha daladala cha Wingwi Mapofu.

iii. Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuchukua jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ukuta, uwekaji wa taa za umeme wa jua (solar) na uandaaji wa eneo (landscaping) kwenye eneo maalum la wajasiriamali Tumbe.

## BARAZA LA MJI WETE

### Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali

Mradi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali kupitia fedha za ahueni ya UVIKO 19 kwa upande wa Baraza la Mji Wete umejengwa katika eneo la Kifumbikai. Mjenzi wa mradi huo ni Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) na Mshauri Elekezi ni Wakala wa Nyumba Zanzibar (ZBA) ambao wameingia mkataba tarehe 13/02/2022 na Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa utekelezaji wa shughuli za mradi. Jumla ya TZS 1,256,119,100 ziliidhinishwa na hadi kufikia Oktoba 2022 jumla ya TZS 999,999,999.70 zimelipwa na mradi ulifikia 75% ya utekelezaji.

### Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Daladala

Jumla ya TZS 30,000,000 zilipangwa kutekeleza mradi wa vituo vya daladala katika maeneo ya Mzambarau Karim, Kangagani, Kidundo, Madenjani, njia ya kuelekea Konde, njia ya kuelekea Chake Chake, na njia ya kuelekea Maziwani. Hadi kufikia mwezi wa Oktoba 2022 mkataba wa kutekeleza mradi huo bado ulikuwa kwa Mwanasheria Mkuu.

### Changamoto Zilizobainika

i. Upandaji wa bei kwa baadhi ya vifaa vya ujenzi kama vile Nondo, mabati na mbao.
ii. Ongezeko la makato ya vifaa vya ujenzi ambapo hapo awali hayakuainishwa makato yake.

**Maoani na ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa inayotekelezwa kwa fedha maalum kama hiyo ya maeneo maalum ya wajasiriamali na masoko kusamehewa kodi za vifaa ili kuondoa changamoto ya uhaba wa fedha.
ii. Kamati inashauri katika kufanya tathmini ya mahitaji (needs assessment) ni muhimu kusikiliza maoni ya wananchi ili kuweza kujua nini kinahitajika kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi wa eneo husika katika utekelezaji wake.

BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

**Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali**

Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum ya Wajasiriamali kwa upande wa Baraza la Mji Chake Chake umefanyika katika eneo la Michakaini. Mshauri Elekezi alikuwa ni Wakala wa Majengo Zanzibar na Mkandarasi ni Kikosi cha Kujenga Uchumi (JKU). Jumla ya TZS 1,176,746,183 zilitengwa kwa ajili ya mradi huo na hadi kufikia Oktoba 2022 hatua ya ujenzi ulifikia 75%.

**Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki na Mboga Mboga Machomane**

Soko la Samaki na Mboga Mboga Machomane ni miongoni mwa miradi iliyomo katika Programu ya Miradi ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (Public, Private Partnership). Fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko hili ni makusanyo ya ndani ambapo jumla ya TZS. 180,000,000 zilitengwa kwa mwaka 2022/2023. Kwa upande wa Wizara imechangia jumla ya TZS 400,000,000 kwa ajili ya Ujenzi wa soko hilo.

Makadirio ya ujenzi ni jumla ya TZS 1,053,441,360.98 ambapo hadi kufikia Oktoba 2022 TZS 421,376,544.40 zimetumika sawa na 40% na asilimia ya utekelezaji ni 75. Mkandarasi wa mradi ni Comfix & Engineering Co na Mshauri

Elekezi ni Wakala wa Majengo Zanzibar.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kamati imegundua kuwa idadi ya vyoo sita (6) ni ndogo ukilinganisha na mahitaji ya watu kwenye maeneo hususan ya soko kwa vile kunakuwa na watumiaji wengi.

### Maoani na Ushauri wa Kamati.

i. Kamati inaishauri Wizara kusimamia vyema Halmashauri zake katika utekelezaji wa miradi kwani imebainika kuwa kumejitokeza mapungufu ya usimamizi licha ya kuwa miradi inaendelea kutekelezwa.

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MKOANI

### Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali

Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani imetekeleza Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali katika eneo la Kipitacho ambapo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ndio Msimamizi wa Mradi huu. Mradi ulianza Febuari 2022 chini ya Mkandarasi Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) na Mshauri Elekezi ni Wakala wa Majengo Zanzibar. Jumla ya TZS 1,176,746,183 zilitengwa na hadi kufikia Oktoba 2022 utekelezaji wa mradi ulifikia asilimia 78.

### Mradi wa Ujenzi wa Masoko

Mradi wa Ujenzi wa Masoko kwa Baraza la Mji Mkoani kwa mwaka 2022/2023 unatekelezwa katika maeneo matatu ambayo ni Mtambile, Kengeja na Ukutini.

Soko la Mtambile na Kengeja hadi kufikia Oktoba 2022 yamefikia katika hatua ya kusafisha maeneo na kuandaa mchoro na hatua za kutafuta mkopo zikiendelea kutoka benki ya NMB.

Soko la Ukutini lilianza ujenzi kwa nguvu za wananchi na kuendelezwa na Baraza la Mji Mkoani kwa hatua ya kuezekwa na umaliziaji (finishing). Hadi kufikia Oktoba 2022 Mkandarasi alikabidhiwa kazi ya kumalizia ujenzi huo na jumla ya

TZS 57,620,175 zimekadiriwa kutumika.

**Mradi wa Maegesho ya Gari (Parking)**

Mradi wa Maegesho ya Gari Baraza la Mji Mkoani (Mkoani Complex) hadi kufikia Oktoba 2022 upo katika hatua ya kuandaa michoro. Kwa mwaka 2022/2023 hakuna fedha zilizotengwa.

**Mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa Umoja ni Nguvu Mkoani**

Mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa Umoja ni Nguvu Mkoani umetekelezwa na hadi kufikia Oktoba 2022 jumla ya TZS 672,742,780 zimetumika ambapo Baraza la Mji Mkoani lilitoa jumla ya TZS 40,000,000 na kilichobaki kilitolewa na Afisi ya Rais - Fedha na Mipango.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kutopata fedha kwa wakati hususan kwenye kumalizia ujenzi na uwekaji wa samani katika Mradi wa Ukumbi wa Umoja ni Nguvu.

ii. Kwenye Ujenzi wa Ukumbi wa Umoja ni Nguvu Mkoani kumejitokeza changamoto kwa Mkandarasi kufanya kazi ambazo hazimo katika mkataba na zilizokuwa kwenye mkataba kuachwa.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inashauri mchakato wa kutafuta wakandarasi uwe unafanyika kwa kufuata utaratibu na kutafuta wakandarasi wenye uweledi kwa miradi inayotarajiwa kutekelezwa kama ya ujenzi wa masoko ya Mtambile na Kengeja.

ii. Kamati inalishauri Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha linafanya mchakato wa kutafuta fedha hata kwa mkopo ili kukamilisha kujenga uzio na kuweka samani kwenye ukumbi wa Umoja ni Nguvu.

iii. Kamati inalishauri Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha linawasimamia vyema wakandarasi waliowachagua katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ili kujenga kwa mujibu wa makubaliano.

**MANISPAA YA MJINI**

## Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali

Manispaa ya Mjini imepata jumla ya TZS 1,000,000,000 ikiwa ni mgao wa fedha za ahueni ya UVIKO 19 ambazo ni kwa ajili ya ujenzi wa mabanda ya wajasiriali wa mbao, gereji na wachomeaji "welding" katika maeneo ya Karakana na Masumbani ikiwa mabanda hayo yana uwezo wa kuchukuwa wastani wa wajasiriamali 300. Ujenzi huo umeshakamilika na jumla ya TZS 750, 000,000 zimetumika na bakaa ya TZS 150,000,000 imekusudiwa kuwajengea wafua vyuma wa Mlandege.

## Mradi wa Ujenzi wa Masoko na Maegesho

Manispaa ya Mjini limetekeleza Mradi wa Ujenzi wa Soko kwa kulifanyia ukarabati mkubwa soko la Darajani ambao umegharimu jumla ya TZS 402,000,000 ikiwa ni fedha za makusanyo ya ndani.

Kwa upande wa maegesho mchakato wa michoro umekamilika na uzio umeshazungushwa katika eneo husika Malindi. Mradi huu utaendeshwa kwa mfumo wa Ubia (PPP) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF).

## Mradi wa Ujenzi wa Maduka

Mradi wa Ujenzi wa Maduka Maeneo ya Darajani unatekelezwa kwa mfumo wa Ubia (PPP) kwa njia ya "Building, Operate and Transfer" (BOT). Ujenzi huo unatarajiwa kufanyika kwa kipindi cha miaka miwili na utakuwa na jumla ya maduka 600 ambayo yatakuwa chini ya mwekezaji kwa kipindi cha miaka 25 ikiwa Mwekezaji huyo atapata asilimi 75 na Manispaa watapata asilimia 25 ya makusanyo.

Kwa hatua ya mwanzo ya ujenzi wa maduka 450 umekamilika kwa asilimia 96.

## Changamoto Zilizobainika

i. Kamati imepata mashaka ya muendelezo wa kuboresha maeneo maalum ya wajasiriamali katika maeneo mbali mbali.

ii. Kwenye ujenzi wa eneo la maegesho hapo Malindi kuna changamoto ya kuharibu urithi wa Mji Mkongwe unaosimamiwa na UNESCO.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kuwa ujenzi wa maeneo ya wajasiriamali uwe endelevu kwa kuzingatia mahitaji sahihi ili kuepuka kujenga majengo ambayo hayatokuwa na matumizi.

ii. Kamati inaishauri Manispaa ya Mjini kufanya tathmini ili kujua athari iwapo fedha za UNESCO zitakosekana kabla na baada ya kumaliza mradi wa maegesho eneo la Malindi.

iii. Kamati imeshauri kufanyika kwa tahmini ili kuweza kujua makisio ya mapato kabla na baada ya ujenzi wa maduka ya Darajani.

## MANISPAA YA MAGHARIBI ‘A’

### Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali

Manispaa ya Magharibi ‘A’ ilipata jumla ya TZS 1,000,000,000. Kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Soko la Munduli na kutumia jumla ya TZS 985,131,868 ikiwa ni gharama za ujenzi huo, ujenzi ulianza tarehe 10/02/2022 na kumalizika tarehe 10/11/2022 kwa usimamizi wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ambae ameshakbidhi kwa Afisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi na mnufaika ambaye ni Manispaa ya Magharibi “A” imeshawapanga wajasiriamali na biashara zinaendelea.

### Mradi wa Ujenzi wa Masoko na Maegesho

Manispaa ya Magharibi ‘A’ lilifunga mkataba na kampuni ya Bi Power Worldwide Limited tarehe 17 Januari 2022 kwa ajili ya ujenzi wa soko na kituo cha daladala Chuini. Mkataba huo ulivunjwa tarehe 06 Juni 2022 kutokana na uwezo mdogo wa mkandarasi. Kwa sasa soko la Chuini linajengwa na Jeshi la Kujenga Uchumi kwa gharama ya TZS 32,071,182,000.17.

Kwa kuanza ujenzi huo Jeshi la Kujenga Uchumi limeshapatiwa jumla ya TZS

6,863,909,871.19 za mkopo wa ahueni ya UVIKO 19 kutoka CRDB.

Kwa upande wa soko dogo la Kwa Kisasi, ujenzi unaendelea na unatarajiwa kugharimu jumla ya TZS 96,656,084 fedha ambazo zitatokana na mapato ya ndani, soko hilo linatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi wa Machi 2023 na kuchukuwa wajasiriamali 40 wakiwemo wa samaki na mboga mboga.

### Mradi wa Kituo cha Daladala Kizimbani

Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Daladala katika eneo la Kizimbani umeanza na utagharimu TZS 607,557,059 kutoka Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na hadi sasa jumla ya TZS 300,000,000 tayari zimeshatolewa na ujenzi umeshaanza kwa hatua za awali na kituo kinatarajiwa kumalizika mwishoni wa mwezi Aprili 2023.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kamati imegundua changamoto ya kuanza kwa mradi wa soko la Chuini huku mkandarasi akiwa hana uwezo wa kifedha wa kutekeleza mradi huo.

ii. Kamati imegundua kuwepo kwa ukusanyaji mdogo wa mapato ya ndani ambayo yanatarajiwa kutumika kwa ajili ya ujenzi wa soko la Kwa Kisasi

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaipongeza Manispaa ya Magharibi ‘A’ kwa kumaliza Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum ya Wajasiriamali huko Munduli.

ii. Kwenye Mradi wa Ujenzi wa Soko huko Chuini Kamati inalishauri Manispaa ya Magharibi ‘A’ kusimamia ujenzi wa soko hilo kwa kufuata taratibu husika ili kuwezesha kumaliza mradi huo kwa muda uliopangwa.

iii. Kamati inalishauri Manispaa ya Magharibi ‘A’ kuhakikisha linakuwa na vianzio vya mapato ya uhakika na yenye kuakisi uhalisia kwenye ukusanyaji wa mapato ili kutekeleza miradi yake.

## MANISPAA YA MAGHARIBI ‘B’

### Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali Mombasa

Mradi wa Jengo la Wajasiriamali Mombasa ni wa ghorofa tatu lenye mita za mraba 623, ambalo litakuwa na jumla ya maduka 96 ambalo linatarajia kuwa na uwezo wa kuchukua wastani wa wafanyabiashara 480 baada ya kumalizika kwake.

Gharama ya ujenzi wa jengo lote ni TZS 3,861,984, 477.57. Gharama za ujenzi kwa awamu ya kwanza ni TZS 1,073,084,356.

### Mradi wa Ujenzi wa Soko la Mwanakwerekwe na Jumbi

Mradi wa Ujenzi wa Soko la Mwanakwerekwe na Jumbi umeanza kwa hatua za awali za kuondoa taka na kujaza kifusi kwenye maeneo husika ya ujenzi wa masoko hayo. Ujenzi wa masoko haya upo chini ya mkandarasi Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) baada ya mkandarasi wa awali kushindwa kuendeleza ujenzi huo.

Mradi wa Ujenzi wa Masoko hayo unategemea fedha za mkopo kutoka benki ya CRDB. Fedha za awali za mkopo usio na riba ni TZS 9,424,052,834.81 ambapo kwa soko la Mwanakwerekwe ni TZS 6,948,278,780.55 na kwa soko la Jumbi ni TZS 2,475,774,054.26. Na fedha za awamu ya pili yenye masharti ya mkopo wa biashara ni TZS 28,278,123,941.19 ambapo kwa soko la Mwanakwerekwe ni TZS 20,849,234,610.45 na kwa soko la Jumbi ni TZS 7,428,889,330.74.

### Changamoto Zilizobainika

i. Katika Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa wajasiriamali, jengo ghorofa 3 na lenye mita za mraba 623 limegharimu TZS TZS 3,861,984, 477.57, sawa na TZS 6,199,012 kwa kila mita moja ya mraba. Gharama hii ni kubwa mno.
ii. Kamati imegundua kuwa kuna ukosefu wa fedha za kukamilisha sehemu ya jengo la wajasiriamali iliyobakia kwa vile fedha zilizotumika awamu ya mwanzo ni za ahueni ya UVIKO 19 na muda wake umeisha.
iii. Udogo wa eneo la Mombasa na lipo karibu mno na barabara kwa harakati za biashara na kupelekea kukosekana kwa eneo la maegesho.

iv. Kwa upande wa masoko ya Mwanakwerekwe na Jumbi ujenzi ulichelewa kutokana na uchelewaji wa fedha za miradi hiyo
v. Upatikanaji wa kifusi kwa ajili ya kuweka sawa ardhi umekuwa mgumu kwa soko la Jumbi.
vi. Kwa kuwa masoko ya Mwanakwerekwe na Jumbi hayatumiki na kupelekea kuwepo kwa soko ya muda Mwanakwerekwe C, Kamati imegundua changamoto ya ukosefu wa miundombinu kwenye soko hilo la muda.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Afisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na na Idara Maalum za SMZ kupitia upya mkataba wa Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum ili kubaini gharama halisi za mradi kwa kuangalia thamani ya fedha.
ii. Kamati inashauri kufanyika kwa jitihada za kuongeza eneo ili kuondoa usumbufu wa nafasi za maegesho utakaojitokeza pindi harakati za biashara zitakapoanza katika eneo la wajasiriamali hapo Mombasa.
iii. Kamati inalishauri Manispaa ya Magharibi 'B' kwa kushirikiana na wadau wengine Serikalini kutafuta fedha kwa ajili ya kuendeleza eneo la wajasiriamali hapo Mombasa.
iv. Kamati inashauri fedha za utekelezaji wa Mradi wa Masoko ya Jumbi na Mwanakwereke kutumiwa ipasavyo kwa mujibu wa mahitaji sahihi kwa ujenzi wa masoko hayo.
v. Kamati inashauri kutafutwa kwa mshauri elekezi kwenye Miradi ya Ujenzi wa Masoko ya Jumbi na Mwanakwerekwe.
vi. Kamati inashauri soko la muda kuboreshwa na kuwekwa mazingira rafiki kwa watumiaji kwa vile hali ya sasa hairidhishi hata kidogo.

**BARAZA LA MJI KATI**

**Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali Hanywega**

Jumla ya TZS 1,000,000,000 za ahueni ya UVIKO 19 zilitengwa kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Maeneo ya Wajasiriamali Hanyegwa. Ujenzi huo umefanywa na Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji Zanzibar chini ya usimamizi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kushirikiana na Baraza la Mji Kati. Ujenzi huo unajumuisha ujenzi wa majengo ya gereji, maduka, sehemu za kuuzia mbao, Sehemu za kuchomea (Welding) na Vyoo. Hadi kufikia Januari 2023, ujenzi wa eneo hilo ulikuwa umefikia hatua za mwisho za kukamilika kwake.

**Mradi wa Ujenzi wa Soko la Wananchi Dunga**

Mradi wa Ujenzi Ujenzi wa Soko la Wananchi Dunga umekamilika na tayari wajasiriamali 32 wameanza kuendesha shughuli zao katika soko hilo.

Mradi wa soko hilo ulikadiriwa kutumia jumla ya TZS 450,000,000 hadi kukamilika kwake. Jumla ya TZS 385,441,420 zimetumika kukamilisha ujenzi huo. Hata hivyo, kuna deni la vifaa TZS 84,118,000 na kufanya jumla ya fedha 469,559,420 zilizotumika kwa ajili ya ujenzi. Kamati ilielezwa kwamba, ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa baadhi ya huduma nyengine za ujenzi ambazo hazikuwemo hapo awali.

**Mradi wa Ujenzi wa Soko la Kikungwi**

Mradi wa ujenzi wa soko la kikungwi ni kwa ajili ya wajasiriamali wa mazao ya baharini ambao wengi wao nia akina mama. Mradi huu kwa mwaka 2022/2023 umepangiwa jumla ya TZS 289,376,800 ila hadi mradi huo upo katika mchakato wa kumtafuta Mkandarasi.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kamati imebaini changamoto ya wafanyabiashara kutokuwa na mwamko wa kutumia soko lililojengwa la Dunga.

ii. Kutuama kwa maji katika baadhi ya maeneo ya soko la Dunga pamoja na kukosekana kwa maji kwa matumizi mbalimbali ya kibinaadamu.

iii. Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa makusanyo ya ndani kwa Baraza hilo

jambo ambalo limerejesha nyuma utekelezaji wa miradi inayotegemea fedha za ndani.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inashauri kuundwa kwa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Eneo la Dunga na kujenga umoja wa wafanyabiashara utakaopelekea mshikamano katika utendaji wa biashara zao.

ii. Kamati inashauri kuundwa kwa kamati ndogo itakayoweza kuwashirikisha wafanyabiashara katika masuala ya utoaji elimu na kuwashajihisha kufanya biashara zao ndani ya soko la Dunga.

iii. Kamati inalishauri Baraza la Mji Kati kuwa na vyanzo vya mapato vyenye uhakika vitakavyoweza kuipatia Baraza hilo mapato.

iv. Kamati inashauri kufanyiwa maboresho maeneo ya ndani ya soko la Dunga ambayo yanaweka maji pamoja kutafuta ufumbuzi wa tatizo la maji kwa matumizi ya kibinaadamu sokoni hapo.

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI

### Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali Kitogani

Mradi wa Ujenzi wa Eneo Maalum la Wajasiriamali kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini umetokana na fedha za ahuweni ya UVIKO 19. Mradi huu upo katika eneo la Kitogani, hadi kukamilika kwake unatarajiwa kutumia TZS 1,915,424,613. Mkandarasi wa Mradi huu ni Kikosi cha Zimamoto ambapo ujenzi ulianza tarehe 09/02/2022 na hadi kufikia Disemba 2022 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 99. Jumla ya fedha zilizolipwa ni TZS 1,786,370,304 sawa na asilimia 93 ya fedha zote zilizotengwa.

### Mradi wa Ujenzi wa Maegesho ya Gari Michamvi

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini ipo katika utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Maegesho ya Gari huko Michamvi kupitia makusanyo yake ya ndani. Mkandarasi wa ujenzi wa maegesho hayo ni AMOS CONSTRUCTION LTD

amabae amefunga mkataba ulioanza tarehe 16/6/2022 na kutakiwa kumaliza tarehe 16/9/2022 ukiwa na thamani ya TZS 210,255,350 kwa ujenzi wote. Mradi tayari umekamilika kwa asilimia 85 ambapo jumla ya TZS 180,486,539 sawa na 86% tayari amelipwa mkandarasi.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kamati imebaini kuwa mradi umechelewa kumalizika kwa wakati uliopangwa.
ii. Kamati imebaini kuwepo na changamoto ya kutofanyika vikao vya mashauriano ya ujenzi (site meeting).

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inalishauri Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kuhakikisha Mkandarasi anamaliza Ujenzi wa Maegesho ya Gari huko Michamvi bila kuongeza muda kamamkataba unavyoelekeza.
ii. Kamati inashauri kuwa Mkandarasi, Mshauri Elekezi na Kamati ya Ujenzi ya Halmashauri kuhakikisha wanafanya vikao vya mashauriano ya ujenzi (site meeting) kwa utaratibu ulio sahihi ili kuepusha changamoto za uchelewaji wa mradi.

**BARAZA LA MJI KASKAZINI ‘A’**

**Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali Pale Kiongole na Ras Nungwi**

Miradi miwili ya Ujenzi wa Maeneo Maalum ya Wajasiriamali ambayo imetekelezwa kupitia fedha za UVIKO 19 kwa jumla ya TZS 853,350,472. Kituo cha Wajasiriamali eneo la Pale Kiongele kimetumia jumla ya TZS 599,563,482 na Kituo cha Wajasiriamali Ras Nungwi kimetumia jumla ya TZS 253,786,990. Aidha, Baraza lipo katika hatua ya kufunga Mkataba na Chuo cha Mafunzo cha Zanzibar kwa ajili ya ujenzi wa mabanda ya mnada na uchimbaji wa kisima katika kituo cha Pale Kiongele ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa urahisi. Ujenzi huu unatarajia kugharimu jumla ya TZS 29,809,600

Tathmini ya fidia kwa wananchi 19 wa eneo la Pale Kiongele imefanyika na jumla ya TZS 61,665,000 zimetengwa. Jumla ya wananchi 16 wamelipwa fidia kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Unguja ambayo imegharimu TZS 37,445,525 sawa na asilimia 60.72% na kwa upande wa Baraza litamalizia TZS 24,219,475 kwa ajili ya kumalizia fidia iliyobakia sawa na asilimia 39.28%.

### Mradi wa Ujenzi wa Masoko ya Chaani, Mkwajuni na soko la Mamalishe Kinyasini

Soko la Mkwajuni lenye ukubwa wa eneo wa mita za mraba 4200, upana mita 60 na urefu mita 70. Ujenzi wa Soko hili unakadiriwa kugharimu jumla ya TZS 1,153,058,431.2 kati ya hizo TZS 441,372,774 ni kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa soko hilo na TZS 711,685,657.2 ni kwa ajili ya ujenzi wa Soko hilo. Jumla ya wanachi 21 kati ya wananchi 32 wameshalipwa fidia na jumla ya TZS 382,977,456 zimetumika kwa ulipaji fidia kati ya TZS 441,372,774 ambazo ni sawa na 86.76% ya fidia. Baraza limeshafunga Mkataba wa ujenzi wa Soko la Mkwajuni wa TZS 711,685,657.2 na Mkandarasi ambae ni Chuo cha Mafunzo kwa ajili kuanza ujenzi huo.

Soko la Chaani linatarajiwa kuwa na ukubwa wa eneo wa mita za mraba 1250, upana mita 25 na urefu mita 50. Baraza la Mji limeshaandaa mchoro pamoja na gharama zake hadi kumalizika kwa ujenzi unaokadiriwa kugharimu jumla TZS 1,335,394,950. Pia Mradi huu unategemewa kutekelezwa kwa awamu mbili (Two Phase), na tathmini ya jengo kwa awamu ya kwanza (phase 1) imekamilika ambayo makisio ya ujenzi wake ni TZS 450,699,846.

Mkataba wa ujenzi wa Soko la Mamalishe Kinyasini umefungwa rasmi tarehe 25 Julai, 2022 baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Kampuni ya RANS Company Limited. Hadi kumalizika kwake ujenzi huu unakadiriwa kugharimu jumla ya TZS 595,351,000/= na hadi kufikia Januari 2023 ujenzi huu umefikia asilimia 44% ya utekelezaji wake.

### Changamoto Zilizobainika

i. Fidia imelipwa kwa baadhi ya wananchi na wengine bado hawajalipwa.

ii. Kuna mafungu ya fedha ambayo ndio yangetumika kwenye utekelezaji wa miradi hayapo kabisa kwenye bajeti na vile vile kuna baadhi ya mafungu yamemaliza fedha na kuhitaji kufanyiwa uhaulishaji (reallocation) kutoka mafungu mengine.
iii. Upungufu wa maji ni tatizo ambalo limesababishwa na nguvu ndogo ya maji kupitia laini ya ZAWA.
iv. Kuchelewa kuanza kazi kwa ruti ya gari kumepelekea kuchelewa kuanza kutumika kwa kituo cha Pale Kiongole.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inashauri kufayike kwa jitihada maalum za upatikanaji wa maji kwenye maeneo yanayotarajiwa kupelekwa kwa wajasiria mali.
ii. Kamati inalishauri Baraza la Mji Kaskazini 'A' iombe ufafanuzi Afisi ya Rais - Fedha na Mipango wa namna ya kuongeza mafungu (Supplimentary budget) na kufanya uhaulishaji (reallocation) wa fedha kwenye mafungu yaliyopungua.
iii. Kamati inalishauri Baraza la Mji Kaskazini 'A' kuhakikisha linaanzisha ruti ya gari Pale Kiongole ili kurahisisha usafiri kwa eneo hilo.
iv. Kamati inalipongeza Baraza la Mji Kaskazini 'A' kwa jitihada zake za kufanikisha hatua tofauti za ujenzi wa miradi ikiwemo pia kujenga utayari wa wajasiriamali kuhamia kwenye maeneo tengefu kwa ajili yao.

## BARAZA LA MJI KASKAZINI 'B'

**Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali Kinduni na Kiwengwa**

Baraza la Mji Kaskazini 'B' kupitia fedha za ahueni ya UVIKO 19 limejenga Maeneo Maalumu ya Wajasiriamali katika eneo la Kinduni lenye ukubwa wa hekari 2.18 na eneo la Kiwengwa lenye ukubwa wa hekari 2.09. Mkandarasi wa ujenzi ni Chuo cha Mafunzo Zanzibar ambae alipatiwa jumla ya TZS 800,493,150.00 kwa mradi wa Kinduni na TZS 288,653,150.00 kwa mradi wa Kiwengwa. Miradi imekamilika na kuzinduliwa rasmi.

### Mradi wa Ujenzi wa Masoko na Maegesho

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Baraza limepanga kujenga Masoko matatu madogo ya wajasiriamali katika maeneo ya Kiwengwa, Kitope na soko dogo la mnada wa Samaki Mangapwani. Utekelezaji wa kazi za ujenzi wa masoko hayo unafanyika katika robo ya tatu ya utekelezaji Januari - Machi 2023 kulingana na mpango kazi wa utekelezaji wa Baraza la Mji.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kamati imegundua kuwa soko la wajasiriamali huko Kiwengwa ni dogo kulinganisha na uhitaji na idadi ya watu waliopo.
ii. Muitikio mdogo wa wajasiriamali kutumia maeneo maalum yaliyojengwa kwa ajili yao.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inashauri kuwa kwenye miradi mikubwa ya maendeleo ya wananchi na nchi kwa ujumla kufanyike upembuzi yakinifu pamoja tathmini ya mahitaji ili utekelezaji wa miradi uwe na ufanisi.
ii. Kamati inashauri Baraza la Mji Kaskazini 'B' kuunda jumuiya ya wafanyabiashara wa eneo la Kiwengwa na kujitahidi kuwashajihisha wajasiriamali kutumia maeneo yaliyotengwa.

### Maoni ya Ujumla

i. Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuandaa mchanganuo wa matumizi ya fedha za ahueni ya UVICO 19 ili kutoa picha halisi ya kilichopangwa na kilichotumika.
ii. Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuandaa miongozo ya matumizi ya masoko kwa kuzingatia mazingira ya masoko hayo na mahali yalipo.
iii. Kamati inaisisitiza Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kutochelewesha marejesho ya mapato yanayoingia Mfuko Mkuu ambayo yanakusanywa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
iv. Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara

Maalum za SMZ kufanya tathmini ya uhitaji wa watendaji kwenye halmashauri zote ili kuongeza watendaji kwenye halmashauri zenye uhitaji wa watendaji.

v. Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kuzifanyia makadirio ya ukusanyaji wa mapato halmashauri zote kwa kuzingatia vigezo vinavyoendana na uhalisia wa vianzio vya mapato kwani kuna baadhi ya vianzio havina uhalisia kwenye ukusanyaji wa mapato ukilinganisha na makadirio yaliyopangwa.

vi. Kamati inashauri katika miradi yote inayotekelezwa kuzingatiwe mahitaji ya watu wenye mahitaji maalum na kama hakuna miundombinu kwa watu wenye mahitaji maalum basi jitihada mahsusi zichukuliwe kuweka miundombinu rafiki kwao.

## TATHMINI YA HALI YA UKUSANYAJI WA MAPATO YATOKANAYO NA TOZO ZA MAEGESHO YALIYOPO KATIKA WILAYA YA MJINI HUSUSAN MAENEO YA MASOKO NA MAENEO MAALUM YA MAEGESHO

Kamati ya Bajeti katika kutekeleza majukumu yake ilipata fursa ya kukutana na Manispaa ya Mjini kwa lengo la kupokea taarifa ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na tozo za maegesho yaliyopo katika Wilaya ya Mjini ikijumuisha maeneo maalum kama vile eneo la maegesho Darajani, Vuga, Kisiwandui, SUZA - Vuga, Malindi uwanja wa Mpira na Polisi, Forodhani na kadhaalika. Katika utekelezaji wa majukumu yake Manispaa ya Mjini limeingia mkataba wa ubinafsishaji wa huduma ya maegesho kwa muda wa miaka mitatu na Kampuni ya ECONEX katika maeneo yote ya Manispaa ya Mjini ambapo mkataba huo ulianza mwaka 2019 na kumaliza muda wake mwaka 2022. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Manispaa ya Mjini kwa kushirikiana na Kampuni ya ECONEX ilikusanya jumla ya shilingi 976,227,500 ikiwa ni ada ya maegesho. Katika fedha hizo, Manispaa ya Mjini liliingiza jumla ya shilingi 585,735,800 sawa na asilimia 60 ya makusanyo na kampuni ya ECONEX ilipata jumla ya shilingi 390,491,700 sawa na asilimia 40 ya makusanyo hayo.

### Changamoto Zilizobainika

i. Mashirikaiano madogo katika ukusanyaji wa ada za maegesho baina ya watendaji wa kampuni ya ECONEX hali ambayo inatoa fursa kwa baadhi ya wananchi kukwepa kulipa ada hizo.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Manispaa ya Mjini kuimarisha na kuhakikisha miundombinu ya lazima inapatikana katika maeneo yote ya maegesho.

ii. Kwa lengo la kuongeza mapato na kuongeza ajira katika Malaka za Serikali za Mitaa, Kamati inashauri Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na Malaka za Serikali za Mitaa zote Unguja na Pemba kuanza taratibu za kukusanya wenyewe mapato katika maeneo ya maegesho ya gari na masoko. Jambo hili linahitaji kuwa na watendaji wenye weledi wa ukusanyaji mapato sambamba na kutumia mfumo wa ukusanyi mapato wa kielektroniki ili kuzuia uvujaji wa mapato hayo.

## TATHMINI YA HALI YA UKUSANYAJI WA MAPATO YATOKANAYO NA BIASHARA NA HUDUMA ZITOLEWAZO KATIKA ENEO LA FORODHANI KWA MWAKA 2021/2022

Bustani ya Forodhani ilianzishwa mwaka 1936 ambapo hapo awali ilijulikana kwa jina la Jubilee Gardens ambayo baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 iliitwa Bustani ya Forodhani. Bustani hii ina shughuli nyingi hususan wakati wa jioni ambapo wafanyabiashara wengi hukusanyika kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi na wageni wafikao katika eneo hilo. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano ya pamoja na Agha Khan Trust for Culture (AKTC) iliona umuhimu wa kulikrabati eneo hilo la Bustani baada ya uchakavu uliodumu kwa muda mrefu.

Baada ya kukarabati eneo hilo, Rais Msaafu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Amani Abeid Karume alitoa maelekezo kwamba suala

la usimamizi na uwendeshaji wa bustani hiyo utakuwa chini ya Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe, Manispaa ya Mjini pamoja na Shirirka la Agha Khan Trust For Culture.

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, makusanyo yaliyokusudiwa kukusanywa katika eneo hilo ni TZS 156,414,000 ambapo makusanyo halisi ni TZS 105,585,800 sawa na asilimia 67 ya makadirio.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Bustani inakabiliwa na changamoto ya malimbikizo ya madeni ya wafanyabiashara na pia kutowasilisha taarifa zao za malipo kwa uongozi wa bustani.

ii. Uchache wa fedha zinazopatikana kutokana na makusanyo ya mapato ukilinganisha na biashara zinazofanyika katika eneo eneo.

iii. Baadhi ya wafanyabiashara wana uelewa mdogo juu ya namna ya utunzaji wa kumbukumbu za malipo hali inayopelekea kukosekana kwa taarifa sahihi za wafanyabiashara hao.

iv. Kumekuwa na uharibifu wa kimazingira wa bustani hususan kwa wafanyabiashara na wageni wafikao katika eneo hilo, hii imetokana na kutokufuata taratibu na miongozo ya bustani.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Mamlaka inayohusika na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na eneo hilo katika jitihada ya kukabiliana na madeni ya wafanyabiashara, kuandaa mikakati madhubuti ya kuweza kuwafatilia kwa karibu wale wote wanaosadikika kuweka malimbikizo hayo ili makusanyo yaweze kupatikana.

ii. Kamati inaitaka Mamlaka inayohusika na ukusanyaji wa mapato kuwapa elimu wafanyabiashara juu ya umuhimu wa kuhifadhi taarifa hizo pamoja na kutumia mfumo wa kidigitali ili kuweka kumbukumbu za malipo hayo na kusimamiwa vizuri taarifa zake ili ziweze kutumika kwa muda wowote zitakapohitajika.

iii. Katika kuhakikisha matumizi mazuri ya eneo hilo, Kamati inaitaka Mamlaka husika kusimamia maeneo yake pamoja na kuwa na mpango wa muda mrefu wa matumizi ya eneo hilo.

iv. Kwa kuwa kuna mkanganyiko juu ya Taasisi gani inahusika na ukusanyaji wa mapato katika eneo la Forodhani, na wakati wa kupokea taarifa hii hakukuwa na jibu rasmi. Hivyo, Kamati haikuridhishwa na hatua hiyo na inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mtaa na Idara Maalum za SMZ, Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Manispaa ya Mjini ili kuweza kujua taasisi gani ndio yenye dhamana ya ukusanyaji mapato na pia inahusika na usimamizi katika bustani hiyo.

# SEHEMU YA SABA

## HITIMISHO

Naomba nihitimishe kwa kukushukuru Mheshimiwa Spika Zubeir Ali Maulid kwa kuliendesha kwa weledi mkubwa Baraza hili la Wawakilishi. Pia namshukuru Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika kwa kukusaidia vyema katika kutekeleza majukumu yako. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum, Waziri Nchi Afisi ya Rais - Fedha na Mipango, Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir Naibu Waziri Nchi Afisi ya Rais - Fedha na Mipango, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati katika vipindi vyote vya mizunguko ya kazi za Kamati. Nawashukuru pia Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi nyengine zilizofanya kazi na Kamati kwa mashirikiano yao mazuri na hatimae kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kwa upande mwengine, Kamati inatoa shukrani za dhati kabisa kwa taasisi zote pamoja na wadau mbali mbali waliyoalikwa na Kamati wakati wa kutekeleza majukumu yake. Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa taasisi hizo kutekeleza

maagizo na ushauri waliopatiwa ili kuimarisha utendaji wa taasisi hizo na kupatikana kwa matokeo mazuri ya usimamizi wa Kamati kwa taasisi hizo.

Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao muda wote wakati wa kutekeleza shughuli za Kamati.

Kwa kumalizia, Kamati inaishukuru kwa dhati kabisa Afisi ya Baraza la Wawakilishi na watendaji wake wote ambao waliweza kuisaidia Kamati katika kufanikisha kazi zake na kupatikana kwa ripoti yake kwa wakati uliopangwa.